



Samia: Misikiti iwe kitovu cha maadili, mshikamano

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitaka misikiti kuwa kitovu cha malezi ya kiroho na maadili mema katika jamii kwa kuanzisha darsa zinazowashirikisha Waumini wa rika zote.

Amesema misikiti ina jukumu muhimu katika kukuza uelewa wa dini, kuimarisha umoja na upendo, pamoja na kujenga mshikamano miongoni mwa waumini na jamii kwa ujumla.

Rais Samia alitoa wito huo Ijumaa iliopita kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zan-

zibar, Hemed Suleiman Abdulla, wakati wa ufunguzi wa Msikiti wa Quba na madrasa yake, kisiwani Bint Abed, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema misikiti ina nafasi muhimu ya kuwaunganisha Waumini katika ibada, huku ikijenga jamii yenye maadili mema na inayomcha Mwenyezi Mungu.

Aliwataka Waumini wa msikiti huo kuhakikisha darsa zinaanzishwa kwa makundi yote ya umri ili kuimarisha uelewa wa dini, upendo na mshikamano miongoni mwao.

Aidha, Rais Samia alisisitiza umuhimu wa kutunza msikiti huo kwa kuhakikisha usafi wa ndani na nje unazingatiwa ili kuuhifadhi katika hali nzuri na kuuwezesha kutoa huduma kwa waumini kwa muda mrefu, hadi kwa vizazi vijavyo.

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya mvua za vuli zinazotabiriwa kuambatana na El Nino kwa kufuata maelekezo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ikiwemo kuhama maeneo hatarishi.

Historia yaandikwa wahitimu wa kwanza chuo cha Qur'an

Chuo cha Qur'an Tukufu na Masomo ya Kiislamu cha Tandale, kinachomilikiwa na Albaraka Foundation, kimeandika historia kwa kutoa wahitimu wake 18 wa kwanza wa ngazi ya Stashahada, huku Serikali ikihimiza wanawake pia wapewe nafasi ya kupata elimu hiyo.

Akizungumza katika mahafali hayo kwa niaba ya Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wanu Hafidh Amir, Mkurugenzi wa Elimu Msingi wa wizara hiyo, Abdul Maulid, amesema amefurahishwa na hatua iliyofikiwa na chuo hicho, lakini akahoji kutokuwapo kwa wanawake miongoni mwa wahitimu.

"Nimeona wanaume tu wakipata elimu hii. Mkihakikisha walezi wakubwa wa watoto ni akina mama, basi wanawake wakijua haya, kazi yetu itakuwa rahisi zaidi na watoto wetu watakwenda katika njia iliyonyooka," amesema.

Ameiomba Albaraka Foundation kuhakikisha katika mahafali yajayo wanawake pia wanakuwa sehemu ya wahitimu wa chuo hicho.

Kwa upande

wake, Mkurugenzi wa Albaraka Foundation, Sheikh Umar Awadh, amesema kuanzishwa kwa chuo hicho kunatokana na haja ya kupanua fursa za elimu ya juu ya Kiislamu nchini, hususan inayotolewa kwa lugha ya Kiarabu.

Naye Sheikh Mohamed Ali Hassan Mshangama, alifafanua kuwa miongoni mwa masomo ambayo wanafunzi hufundishwa ni pamoja na Kiislamu, yakiwemo Qur'an, Tafsir, Usul na Hadith.

Jambo lililofurahisha ni pale Sheikh Awadh alipofafanua kuwa Albaraka inalenga kuunganisha elimu ya dini na masomo ya kawaida ili wanafunzi wapate sifa na vyeti vinavyotambulika katika mfumo rasmi wa elimu nchini.

Alieleza kuwa utaratibu huo umewaweza baadhi ya wanafunzi waliopitia mfumo wa masomo ya dini kuendelea na elimu ya sekondari hadi kidato cha tano na sita.

Wadau wataja faida

Amir wa Umoja wa Wanazuoni Tanzania

(Hay-atul Ulamaa), Sheikh Abdallah Ndauga, ameyaita mahafali hayo kuwa ya kihistoria, akisema elimu ya Qur'an ndio msingi wa kuwajenga wahitimu wenye maadili mema na uwezo wa kuitumikia jamii.

Naye Amir wa Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA), Ally Zubeir, amesema kuanzishwa kwa chuo hicho ni hatua muhimu katika kuendeleza elimu ya Kiislamu nchini akipongeza juhudi za waasisi wake katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Rais wa Umoja wa Maahad za Kiislamu Tanzania, Ally Nassor Ally, ambaye pia ni Naibu Mudir wa Markaz Kuu ya Ansaar Muslim Youth Centre, Tanga, amesema chuo hicho kimefungua fursa kwa wahitimu wa maahad kuendeleza elimu yao katika ngazi za juu.

Alisema taasisi hizo ni wadau wakubwa wa chuo kwa kuwa baadhi ya wahitimu wao hujiunga nacho, huku akitoa wito wa kupanuliwa kwake na kuongezwa vitivo.

Kwa upande wake, Naibu Mudir wa Maahad Junejd Islamiy ya Zanzibar, Abdulrhman Ally Saggaf, amesema kuanzishwa kwa vyuo vya aina hiyo nchini kunapunguza ulazima wa vijana kusafiri nje ya Tanzania kutafuta elimu ya juu ya Kiislamu.

Alisema kuongezeka kwa vitivo na fursa za masomo ya dini katika chuo hicho kwa miaka ijayo kutakuwa ukombozi mkubwa kwa vijana wanaotamani kuendeleza taaluma zao.

Albaraka Foundation, iliyoanzishwa mwaka 2011, inajihusisha na shughuli za elimu, afya na misaada kwa waathirika wa majanga.





JUMADA AL-AWWAL 9, 1448

حججنا أول



**MATUKIO
KATIKA PICHA**

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

Mahafali Chuo cha Qur'an Tukufu na Masomo ya Kiislamu





Ziara za Mwinyi Qatar, Hispania zafungua milango ya uwekezaji

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema ziara zake nchini Qatar, Hispania na Armenia zimefungua fursa mpya za uwekezaji, maendeleo ya michezo na uhifadhi wa mazingira, akisisitiza umuhimu wa kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa ili kuleta manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar, akirejea kutoka ziara hizo zilizolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika maeneo mbalimbali ya maendeleo.

Amesema ziara hizo zimezaa matokeo yenye matarajio ya kuchochea ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, hususan kupitia uwekezaji wa sekta binafsi, kukuza vipaji vya vijana na kuimarisha juhudi za kukabiliana na changamoto za kimazingira.

Katika ziara yake nchini Qatar,

Dkt. Mwinyi amesema kampuni ya Alfardan imeonesha nia ya kuwekeza Zanzibar, hatua inayoweza kufungua fursa zaidi za kiuchumi, kuongeza shughuli za uwekezaji na kuchangia maendeleo ya visiwa hivyo.

Nia hiyo ya uwekezaji inatajwa kuwa miongoni mwa fursa zinazotokana na diplomasia ya kiuchumi, inayolenga kuvutia mitaji kutoka nje na kuimarisha ushirikiano kati ya Zanzibar na washirika wake wa kimataifa.

Amesema pia makubaliano yaliyofikiwa kati ya Real Madrid Foundation na Unicorn Zanzibar Sports Limited yanalenga kuimarisha maendeleo ya michezo, h a s a

soka, kwa kuibua na kukuza vipaji vya vijana.

Kupitia ushirikiano huo, vijana wa Zanzibar wanatarajiwa kunufaika na fursa za kukuza uwezo wao wa kisoka, huku makocha wa ndani wakipata nafasi ya kuimarisha ujuzi na utaalumu wao. Hatua hiyo inalenga kujenga msingi imara wa maendeleo ya soka na kuongeza uwezo wa Zanzibar kushiriki katika ushindani wa michezo.

Katika ziara yake nchini Armenia, Dkt. Mwinyi amesema amepata fursa ya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika uhifadhi wa mazingira, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kulinda rasilimali za bahari.

Amesitiza kuwa ushirikiano katika maeneo hayo ni muhimu kwa Zanzibar, ambayo inategemea kwa kiasi kikubwa rasilimali za bahari na mazingira katika kuendeleza shughuli za kiuchumi na maisha ya wananchi wake.

Uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari ni maeneo muhimu yanayohitaji ushirikiano wa kimataifa, hususan katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kulinda mifumo ikolojia ya baharini.

Hata hivyo, Rais Dkt. Mwinyi amesisitiza kuwa mafanikio ya ziara hizo hayatapimwa kwa mazungumzo na makubaliano pekee, bali kwa utekelezaji wake na matokeo yatakayopatikana.

Amesema ni muhimu kuhakikisha masuala yote yaliyojadiliwa na makubaliano yaliyofikiwa yanatekelezwa ili kuleta manufaa yanayoonekana kwa wananchi, kukuza uchumi na kuchangia maendeleo ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.



Mtanzania Edha Nahdi aongeza nguvu uwekezaji wa nishati

■ Anunua kampuni
ya mafuta ya Oryx
Energies Tanzania



Kundi la kampuni la Amsons Group, linaloongozwa na mfanyabiashara Mtanzania Edha Nahdi, limesaini makubaliano ya kununua biashara ya mafuta ya Oryx Energies nchini Tanzania kwa thamani inayoripotiwa kufikia dola milioni 230 za Marekani.

Makubaliano hayo yanahusisha biashara ya usambazaji na uuzaji wa mafuta, vituo vya kujazia mafuta, maghala ya kuhifadhi mafuta na miundombinu mingine ya usambazaji.

Katika taarifa yake ya Oktoba 16, 2026, Oryx Energies imethibitisha makubaliano hayo, ikieleza kuwa yanatokana na mapitio ya kimkakati ya shughuli zake barani Afrika.

Hata hivyo, kampuni hiyo haikutaja thamani ya mauziano. Tovuti ya habari za biashara ya Billionaires Africa imeripoti kuwa

makubaliano hayo yana thamani ya takriban dola milioni 230.

Kwa mujibu wa tovuti hiyo, ununuzi ukikamilika utaongeza uwezo wa Amsons kuhifadhi mafuta kutoka tani 300,000 hadi 800,000 na kufikisha mtandao wake wa rejareja kwenye vituo takriban 300 katika nchi mbalimbali.

Taarifa hiyo pia imetaja umiliki wa hisa za Oryx katika kampuni ya Tanzania International Petroleum Reserves (TIPER), inayosimamia ghala kubwa la mafuta jijini Dar es Salaam, kuwa miongoni mwa mali zinazohusika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Energies, Moussa Diao, amesema kampuni yake inaamini Amsons itaendeleza biashara hiyo na kuleta fursa mpya kwa wafanyakazi, wateja na washirika.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Amsons Group, Edha Nahdi, amesema makubaliano hayo ni hatua muhimu katika mpango wa kupanua uwekezaji wa kundi hilo kwenye sekta za nishati na usafirishaji.

Alisema kuunganisha miundombinu ya Oryx na shughuli za Amsons kutasaidia kuimarisha upatikanaji wa mafuta nchini na nafasi ya Tanzania kama kitovu cha usambazaji wa mafuta Afrika Mashariki na Kati.

Amsons tayari imepanua uwekezaji wake katika sekta ya saruji, ikiwemo kununua Bamburi Cement nchini Kenya mwaka 2024.

Hata hivyo, mauziano ya Oryx bado hayajakamilika kisheria. Yanategemea idhini za mamlaka husika na kutimizwa kwa masharti mengine, huku Oryx ikiendelea kutoa huduma zake kama kawaida.

بَيْتُ الْمَالِ

IJUE BAITULMAAL TANZANIA

Waislamu wahimizwa kutoa Zaka kupitia Baitulmaal

DAR ES SALAAM — Waislamu wamehimizwa kutoa Zaka kupitia taasisi za usimamizi wa Zaka badala ya kuigawa binafsi, ili kuhakikisha misaada hiyo inawafikia walengwa wanaostahiki na kuwa na matokeo ya kudumu katika maisha yao.

Wito huo umetolewa na Naibu Afisa Mtendaji wa Baytulmaal Tanzania, Kassim Mohamed, wakati wa kipindi maalumu cha maswali na majibu kilichofanyika kupitia mtandao wa Google Meeting, katika kampeni ya Iijue Baytulmaal Tanzania.

Kassim amesema tofauti kubwa kati ya kutoa Zaka binafsi na kupitia taasisi ni kwamba Baytulmaal hufanya tathmini ya hali ya mhitaji kabla ya kuamua aina ya msaada unaomfaa.

Mohamed alisema: “Mtu anaweza kumpa mhitaji fedha bila kujua mahitaji yake halisi, wakati taasisi huangalia namna msaada huo utakavyoweza kuboresha maisha yake.”

Aliongeza kuwa wanufaika wanaowezeshwa kufanya biashara hupatiwa ushauri wa kiuchumi na kufuatiliwa ili kuhakikisha wanatumia mitaji waliyopewa kwa malengo yaliyokusudiwa na pia kanzidata yake inawaunganisha wahitaji na fursa nyingine, zikiwemo huduma za afya, mafunzo ya ufundi na ufadhili wa masomo.

Alitolea mfano wanafunzi waliounganishwa na fursa za masomo nchini Malaysia kupitia ushirikiano na Tanzania Muslim Professionals Association (TAMPRO).

Wanawake wanatumia vizuri zaidi mitaji ya Zaka kuliko wanaume

DAR ES SALAAM — Baytulmaal Tanzania imesema uzoefu wake katika kuwapatia wahitaji mitaji inayotokana na Zaka unaonyesha kuwa wanawake wamekuwa wakitumia misaada hiyo kwa ufanisi zaidi kuliko wanaume, huku baadhi ya wanaume wakidaiwa kutumia fedha hizo kinyume na malengo waliyoyaeleza.

Akizungumza katika kipindi maalumu cha maswali na majibu cha kampeni ya Iijue Baytulmaal Tanzania, Afisa Mtendaji wa taasisi hiyo, Yusuph Mohamed, amesema tathmini za ufuatiliaji wa wanufaika zimeonyesha tofauti hiyo.

Alisema baadhi ya wanaume wamekuwa wakiomba mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, lakini baada ya kupokea fedha huzielekeza kwenye matumizi mengine, jambo linalokwamisha malengo ya kuwawezesha.

Kwa upande mwingine, amesema wanawake wengi waliopatiwa mitaji wameonyesha matokeo mazuri katika kuendeleza shughuli zao na kusaidia familia.

Kutokana na uzoefu huo, Yusuph alisema Baytulmaal imeanza kuweka mkazo katika kuwaunganisha wanawake kwenye vikundi vya uwezeshaji na kuwapatia elimu ya biashara, hatua inayolenga kuongeza uwezo wao wa kujitegemea na kuboresha ustawi wa familia zao.

Wengi bado wana uelewa usio sahihi kuhusu Zaka

DAR ES SALAAM — Baytulmaal Tanzania imesema bado kuna Waislamu wenye uelewa usio sahihi kuhusu Zaka, huku baadhi yao wakiamini kuwa ni misaada inayotolewa na wahisani kutoka nje ya nchi badala ya kuwa ibada ya lazima kwa Waislamu wanaotimiza masharti yake.

Naibu Afisa Mtendaji wa taasisi hiyo, Kassim Mohamed, alieleza hayo wakati wa kipindi cha maswali na majibu cha kampeni ya Iijue Baytulmaal Tanzania, iliyolenga kuongeza uelewa wa jamii kuhusu Zaka, Sadaka na Wakfu.

Alisema katika shughuli za taasisi hiyo amekutana na Waislamu wanaozifahamu nguzo tano za Uislamu, lakini hawaelewi vizuri maana na utaratibu wa utekelezaji wa Zaka.

Alitolea mfano baadhi ya watu waliokuwa wakidhani kwamba Zaka ni fedha zinazotumwa kutoka nje ya nchi na kugawiwa kwa wananchi kama misaada mingine, dhana ambayo si sahihi kwa sababu Zaka ni haki ya wanaostahiki inayotolewa katika mali za Waislamu waliotimiza masharti yaliyowekwa na Sharia.

Aliongeza kuwa hata baadhi ya wenye biashara na mali hawafahamu kama wamefikia kiwango kinachowawajibisha kutoa Zaka.

Kutokana na changamoto hiyo, Baytulmaal inatoa huduma ya bure ya kukokotoa Zaka kwa wafanyabiashara na watu wenye akiba ili kuwasaidia kutambua wajibu wao. Alisema taasisi hiyo pia inaendesha semina na programu za elimu kwa jamii kuhusu Zaka na Wakfu, akisisitiza kuwa elimu inahitajika kwa watoaji na wapokeaji ili kuhakikisha haki za wahitaji zinawafikia ipasavyo.

Michango ya bima ya Kiislamu Tanzania yaongezeka kwa asilimia 39.8

Soko la bima ya Kiislamu (Takaful) nchini Tanzania limeendelea kukua, huku michango ya washiriki ikiongezeka kwa asilimia 39.8 mwaka 2025, kutoka Shilingi bilioni 4.62 mwaka 2024 hadi Shilingi bilioni 6.50.*

Takwimu hizo zimo katika Taarifa ya 25 ya Utendaji wa Soko la Bima Tanzania kwa mwaka 2025, iliyozinduliwa Oktoba 16, 2026, jijini Dodoma na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA). Akizungumzia mwenendo huo, Kamishna wa Bima na Mtendaji Mkuu wa TIRA, Dkt. Baghayo Saqware, amesema ukuaji huo unaonyesha umuhimu wa kuanzishwa kwa huduma za Takaful ili kukidhi mahitaji ya jamii ya Waislamu.

Takaful ni mfumo wa bima unaofuata misingi ya Sharia, ambapo washiriki huchangia katika mfuko wa pamoja kwa lengo la kusaidiana wanapokumbwa na majanga au hasara zinazokatiwa bima.

Ukuaji huo umejiri wakati sekta nzima ya bima nchini ikirekodi ongezeko la asilimia 68.4 katika ada za bima zilizoandikishwa, kutoka Shilingi trilioni 1.52 mwaka 2024 hadi trilioni 2.55 mwaka 2025.

Wito wa maboresho ya madrasa zetu umekuja wakati sahihi



**Kauli ya Kai-
mu Sheikh wa
Mkoa wa Dar es
Salaam, Sheikh
Abbas Ramad-
han, kuhusu mfu-
mo wa uendesh-
aji wa madrasa
nchini, inapaswa
kuwa chachu ya
mjadala mpana
na wa kina kuhu-
su mustakabali
wa elimu ya dini
ya Kiislamu.**

Wito wa maboresho ya madrasa zetu umekuja wakati sahihi

Kauli ya Kaimu Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Abbas Ramadhan, kuhusu mfumo wa uendeshaji wa madrasa nchini, inapaswa kuwa chachu ya mjadala mpana na wa kina kuhusu mustakabali wa elimu ya dini ya Kiislamu.

Hoja yake kwamba kwa miaka nenda rudi uendeshaji wa madrasa zetu umekuwa uleule wa kizamani, bila mabadiliko yanayoendana na wakati, inagusa ukweli ambao jamii yetu inapaswa kuutazama kwa umakini mkubwa.

Ni kweli zina nafasi muhimu katika malezi ya watoto, kuwajengea maadili, kuwafundisha misingi ya dini na kuwaandaa kuwa watu wenye hofu ya Mwenyezi Mungu, nidhamu na uwajibikaji katika jamii, lakini hiyo sio sababu ya kuendelea na mfumo wa ufundishaji ya kimazoea bila kujali ufanisi katika ulimwengu wa leo.

Hivyo Kauli yako Sheikh Abbas imegusa eneo ambalo kwa muda mrefu linahitaji mjadala wa wazi, wenye nia ya kujenga na usio na hofu ya mabadiliko.

Hatupuuzi juhudi za walimu wa madrasa, walakudharau mchango wa masheikh na walezi waliojitolea kwa miaka mingi kusimamia elimu ya dini. Hata hivyo kazi yao nzuri inapaswa kuendelezwa kwa mbinu bora zaidi zinazokidhi mahitaji ya kizazi cha sasa

Madrasa hazipaswi kubaki kama zili-vyokuwa miaka mingi iliyopita kwa sababu tu ndizo tulizozioea.

Kama tunataka watoto waipende elimu ya dini, wazazi waendeleo kuwaamini walimu na taasisi hizi, na jamii ipate kizazi chenye uelewa mpana, ni lazima tuanze kufikiria upya namna madrasa zina-vyoendeshwa.

Tutoe kwenye mazoea

Kwa miaka mingi, taswira ya madrasa katika maeneo mengi imekuwa ya watoto kukaa chini kwenye majamvi au mikeka, wakisikiliza mwalimu na kujifunza kwa njia ambazo mara nyingi hutegemea zaidi mazoea kuliko ubunifu. Katika baadhi ya maeneo, viboko na

adhabu kali vimekuwa sehemu ya mfumo wa kuwafundisha watoto, kana kwamba bila ukali huo elimu ya dini haiwezi kueleweka.

Niwakatisasawakujiuliza: je, hayandiyomazingira pekee yanayoweza kumlea mtoto katika misingi ya Uislamu? Je, kutumia madawati, vitabu vya kisasa, vifaa vya kufundishia na mbinu shirikishi kunapunguza utukufu wa elimu ya dini? Jibu ni hapana. Elimu ya dini inaweza kutolewa katika mazingira bora, yenye usafi, usalama, nidhamu na vifaa vinavyorahisisha ujifunzaji.

Madrasa inaweza kuwa na madawati, ubao, vitabu vya kutosha, maktaba ndogo na vifaa vya kidijitali pale vinapowezekana. Walimu wanaweza kutumia mjadala, maswali na majibu, kazi za vikundi na mifano inayohusiana na maisha halisi kuwasaidia watoto kuelewa wanachofundishwa.

Hata suala la viboko linahitaji kuangaliwa upya. Nidhamu ni muhimu, lakini haipaswi kuchanganywa na ukatili au adhabu zinazoweza kumuumiza mtoto kimwili na kisaikolojia. Watoto wanahitaji mazingira yanayowafanya wajisikie salama, waheshimiwe na wawe huru kuuliza maswali ili kuelewa zaidi.

Hata hivyo, maboresho ya madrasa haku-maanishi kuiga kila kitu kutoka kwenye mfumo wa elimu ya kawaida bali kuchukua mbinu bora

zinazoweza kuimarisha ufundishaji bila kuondoa utambulisho, maadili na misingi ya dini.

Madrasa ziwe hivi

Mabadiliko tunayoyahitaji hayaishii kwenye madawati na majengo mazuri. Tunataka madrasa zinazomjenga mtoto kwa upana, zikimpa maarifa ya dini na kumsaidia kupata stadi muhimu za maisha.

Mtoto anapojifunza Qur'an, fiqhi, akida na maadili ya Kiislamu, anaweza pia kufundishwa usafi binafsi, utunzaji wa mazingira, mawasiliano mazuri, ushirikiano, uwajibikaji, uongozi na namna ya kutatua changamoto kwa busara. Stadi hizi hazipingani na dini. Kinyume chake, zinaweza kumsaidia mtoto kutekeleza kwa vitendo maadili anayofundishwa.

Kwa mfano, mafundisho kuhusu usafi yanaweza kuambatana na shughuli za kutunza mazingira; mafunzo kuhusu uaminifu yanaweza kujadiliwa kupitia mifano ya maisha ya kila siku; na mafundisho kuhusu mshikamano yanaweza kuimarishwa kwa shughuli za vikundi na kusaidiana.


Pia, madrasa zinaweza kuanzisha shughuli za ziada zinazolingana na umri wa watoto, kama usomaji, uandishi, mawasiliano na maarifa ya msingi ya teknolojia.

Pale rasilimali zinaporuhusu, ushirikiano na wataalamu unaweza kusaidia kuwapa watoto uelewa wa masuala ya afya, mazingira na stadi nyingine zinazohitajika katika maisha ya kisa. Hii haimaanishi madrasa zichukue nafasi ya shule, bali ziongeze thamani katika malezi na maendeleo ya mtoto.

Ili kufanikisha mabadiliko hayo, viongozi wa dini, walimu, wazazi na wadau wengine wanapaswa kukaa pamoja na kuandaa mikakati inayotekelezeka. Wamiliki na wasimamizi wa madrasa wanaweza kuanza na hatua ndogo kulingana na uwezo wao, huku taasisi za dini na wafadhili wakisaidia kuboresha miundombinu, vifaa na mafunzo ya walimu. Ni muhimu pia walimu wa madrasa wapate mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji na malezi ya watoto ili waweze kuwasaidia watoto kuelewa masomo, hata bila kutegemea adhabu. Aidha, wazazi wanapaswa kushirikishwa katika maendeleo ya watoto na tathmini ya ubora wa elimu inayotolewa.

Mwisho wa yote, mafanikio ya madrasa hayatapimwa kwa idadi ya watoto wanaohudhuria pekee, bali pia kwa ubora wa maarifa wanayopata, tabia wanazojenga na uwezo wao wa kutumia mafunzo hayo katika maisha.

Sheikh Abbas amefungua mjadala unaostahili kuendelezwa kwa vitendo. Sasa ni wajibu wa wadau kugeuza mao-no hayo kuwa hatua zinazoonekana. Tukiboresha mazingira ya kujifunzia, tukawaandaa walimu na kupanua wigo wa malezi bila kupoteza misingi ya dini, tutakuwa tumepiga hatua muhimu.



خطبة الجمعة

IMEANDALIWA

Na Barnabas Mkwaju

0766 364 354

MIMBARI ZETU

KUTOKA

Masjid Al-Haram
(Makka)

Masjid Nabawi
(Madina)

Masjid Bukhary
(Morogoro)

Masjid Haqq
(Morogoro)



MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA

IMAMU NA KHATIBU SHEIKH DKT. ABDULLAH BIN AWAD AL-JUHANI



Waislamu watakiwa kuhifadhi Swala tano, kuziswali kwa wakati

MAKKA, Saudi Arabia — Imamu wa Masjid al-Haram, Sheikh Dkt. Abdullah bin Awad Al-Juhani, amewataka Waislamu kuzingatia Swala tano za faradhi, kuziswali kwa wakati na kwa utulivu, akisisitiza kwamba Swala ni msingi muhimu wa dini na kinga dhidi ya maovu.

Akitoa khutba ya Ijumaa, Oktoba 16, 2026, katika Msikiti Mtukufu wa Makka, Sheikh Al-Juhani amesema Muislamu anapaswa kuipa Swala nafasi ya kwanza katika maisha yake badala ya kuiruhusu shughuli ya dunia kumfanya apuuze wajibu huo.

Amesema Swala ni nguzo ya pili ya Uislamu na ni ibada yenye nafasi kubwa katika kupima mwenendo wa mja mbele ya Mwenyezi Mungu.

Akizungumzia namna ya kutekeleza ibada hiyo, Sheikh Al-Juhani amewataka Waislamu kuhakikisha wanatimiza masharti na nguzo za Swala, ikiwemo kujitwahirisha, kuelekea Qibla na kuswali kwa utulivu na unyenyekevu.

Alionya dhidi ya tabia ya kuharakisha Swala kiasi cha kukosa utulivu unaotakiwa katika rukuu na sijda na kwamba Swala haipaswi kutekelezwa kama mazoea ya viungo vya mwili pekee, bali inapaswa kuambatana na moyo ulioelekea kwa Mwenyezi Mungu.

Akirejea Qur'an, Surat Al-Ankabut, aya ya 45, amesema Swala inayotekelezwa ipasavyo humsaidia Muislamu kujiepusha na machafu na maovu.


Aidha, aliwakumbusha Waumini kwamba Mwenyezi Mungu amezi-faradhisha Swala katika nyakati maalumu, kama inavyoelezwa katika Surat An-Nisaa, aya ya 103.

Alisema shughuli za biashara, kazi, michezo na mikusanyiko ya kijamii hazipaswi kutumiwa kama sababu za kuchelewesha Swala mpaka muda wake upite.

Sheikh Al-Juhani aliwahimiza pia wazazi kuwafundisha watoto wao umuhimu wa Swala na kuwajengea utamaduni wa kutekeleza tangu wakiwa wadogo.

MSIKITI WA MTUME, MADINA

IMAM NA KHATIBU SHEIKH DKT. AHMAD BIN ALI AL-HUDHAIFI



Imani ya Siku ya Kiyama hujenga utulivu wa moyo –

MADINA, Saudi Arabia. Imamu wa Msikiti wa Mtume Muhammad (Masjid an-Nabawi), Sheikh Dkt. Ahmad bin Ali Al-Hudhaifi, amesema imani thabiti ya Siku ya Kiyama humjengea Muislamu utulivu wa moyo, uchamungu na uwajibikaji katika kutekeleza haki za Mwenyezi Mungu na wanadamu.

Akitoa khutba ya Ijumaa, Oktoba 16, 2026, mjini Madina, Sheikh Al-Hudhaifi amewahimiza Waislamu kutafakari mafundisho ya Qur'ani kuhusu maisha ya duniani, kifo, kufufuliwa na hesabu ya matendo Siku ya Kiyama.

Amesema mtu anayekumbuka kuwa maisha ya duniani yana mwisho na kwamba atawajibishwa kwa matendo yake huwa na msukumo wa kujiepusha na maovu, kutenda mema na kuheshimu haki za wengine.

Katika khutba hiyo, Sheikh Al-Hudhaifi alielekeza waumini kutafakari mafunzo ya Surat Qaf, akieleza kuwa sura hiyo inabainisha uwezo wa Mwenyezi Mungu wa kuumba viumbe, kuwafufua wafu na kuwahukumu wanadamu kwa matendo yao.

Amesema Qur'ani inawahimiza watu kutafakari uumbaji wa mbinu, ardhi na milima, pamoja na mvua inayohuisha ardhi iliyokauka, akibainisha kuwa dalili hizo zinaonesha uwezo wa Mwenyezi Mungu wa kufufua viumbe baada ya kufa.

Akirejea aya ya 16 ya Surat Qaf, Sheikh Al-Hudhaifi amewakumbusha waumini kuwa Mwenyezi Mungu anamfahamu mwanadamu kwa undani, ikiwa ni pamoja na mawazo na minong'ono ya nafsi yake.

Amesema ujuzi huo wa Mwenyezi Mungu unapaswa kumfanya Muislamu ajichunge katika matendo yake yote, yawe ya wazi au ya siri, kwa kutambua kuwa hakuna jambo linalofichika mbele Yake.

Amehimiza waumini kuimarisha imani yao, kujitathmini na kuji-andaa kwa Siku ya Kiyama kwa kufanya mema na kutekeleza wajibu wao kwa uaminifu.

MSIKITI BUKHARY, MOROGORO

MLINGANIAJI WA KIMATAIFA
SHEIKH NASSOR RAMADHAN



Imani ya Akhera humfanya Muislamu ajiepushe na maasi

MOROGORO. Sheikh Nassor Ramadhan wa Masjid Imaam Bukhary, Kihonda, Morogoro, amewataka Waislamu kuimarisha imani yao kwa Mwenyezi Mungu na Siku ya Kiyama, akisisitiza kuwa kuamini maisha ya Akhera humsaidia mtu kujizuia na maasi na kuishi kwa kufuata mipaka ya dini.

Akitoa khutba ya Ijumaa iliyokuwa na mada Imani nzuri na mbaya, Sheikh Nassor alisema mtazamo wa mtu kuhusu maisha baada ya kifo una nafasi kubwa katika kuamua mwenendo wake na namna anavyowajibika mbele ya Mwenyezi Mungu.

Alieleza kuwa baadhi ya watu hudai kuwa maisha huishia mtu anapokufa, bila kuwepo maisha mengine baada ya dunia. Kwa mujibu wake, mtazamo huo unaweza kumfanya mtu kupuuza wajibu wake wa kidini na kufanya anavyotaka bila kujali matokeo ya matendo yake.

Sheikh Nassor alisisitiza kuwa Muislamu anapaswa kuwa na hofu ya kumuasi Mwenyezi Mungu, akitambua kuwa kila tendo linaweza kuwa na matokeo katika maisha ya Akhera.

Alirejelea kauli “Inni akhafu in ‘asaytu Rabbi”, yenye maana ya “Hakika mimi ninaogopa kumuasi Mola wangu,” akieleza umuhimu wa kuwa na tahadhari dhidi ya matendo yanayoweza kumletea mtu adhabu Siku ya Kiyama.

Alisema mtu anayeamini kuwa atafufuliwa na kuhesabiwa kwa matendo yake anapaswa kujitathmini kabla ya kutenda, kutekeleza yaliyoamrisha na dini na kujiepusha na yaliyokatanzwa.

Akifafanua kuhusu imani, Sheikh Nassor alisema ni yakini iliyo-thibiti moyoni mwa mtu, inayopaswa kuonekana katika mwenendo na matendo yake ya kila siku.

Aliwahimiza Waislamu kuimarisha imani zao kwa kuzingatia mafundisho ya Uislamu na kukumbuka kuwa maisha ya dunia ni kipindi cha maandalizi ya maisha ya Akhera.

MASJID HAQQ, MOROGORO

MLINGANIAJI WA KIMATAIFA
SHEIKH SHABANI DHABAHU



Sheikh Dhabahu: Baba bora ahakikisha watoto wanaswali

MOROGORO. Sheikh Shabani Dhabahu wa Masjid Haqq, Morogoro, amewataka wazazi, hususan baba, kuwalea watoto katika misingi ya dini kwa kuhakikisha wanatekeleza ibada ya swala, akisisitiza kuwa mafanikio ya mtoto hayapaswi kupimwa kwa elimu na mali pekee.

Akitoa khutba ya Ijumaa iliyohusu Baba Bora, Sheikh Dhabahu alisema baba hawezi kujihesabu kuwa amekamilisha wajibu wake wa malezi kwa kumsomesha mtoto katika shule ya gharama kubwa, kumjengea makazi ya kifahari au kumvisha mavazi bora, ikiwa hajamwelekeza katika ibada ya swala.

Alisisitiza kuwa jukumu la baba ni pamoja na kumfundisha mtoto namna sahihi ya kuswali na kufuatilia utekelezaji wa ibada hiyo ili kuhakikisha anafuata misingi inayotakiwa katika Uislamu.

Akirejelea mafundisho ya Mtume Muhammad (Rehema na amani zimshukie), Sheikh Dhabahu alisema watoto wanapaswa kuamrisha kuswali wanapofikisha umri wa miaka saba.

Alisema hatua hiyo ni muhimu katika kumjengea mtoto mazoea ya ibada tangu akiwa mdogo, kabla ya kukua na kuingia katika hatua nyingine za maisha.

“Baba anaamka kwenda kuswali swala ya Alfajiri msikitini, lakini anamwacha mwanawe amelala. Haya ndiyo malezi ya Kiislamu tunayopaswa kuyasimamia?” alihoji, akiwataka wazazi kutafakari namna wanavyotekeleza wajibu wao wa kidini kwa watoto.

Aliongeza kuwa baadhi ya wazazi huamka mapema kuwaandaa watoto kwenda shule, lakini husahau kuhakikisha kuwa wametekeleza swala, jambo linaloonesha umuhimu wa kuweka malezi ya kiroho sambamba na maandalizi ya elimu.

Kwa mujibu wa Sheikh Dhabahu, baba bora anapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika ibada na kuhakikisha watoto wanajifunza dini kwa vitendo, si kwa maneno pekee.

Mawaziri Afrika wavutiwa na maboresho Bandari ya Dar



Bandari ya Dar es Salaam imepongezwa kwa maboresho ya miundombinu yaliyoiongezea uwezo wa kuhudumia meli kubwa na hivyo kuimarisha imani ya nchi za Afrika katika kuitumia kama lango muhimu la biashara ya kikanda na kimataifa.

Pongezi hizo zilitolewa na Mawaziri na Makatibu wakuu wa nchi wanachama wa Shirika la Usafiri wa Majini la Mashariki, Kusini na Kaskazini mwa Afrika (MOESNA) wakieleza kuridhishwa na kukua kwa ufanisi wa huduma bandarini.

Katika ziara hiyo, wajumbe walikagua gati namba sifuri hadi saba, ambapo walishuhudia

shughuli za upakuaji wa magari kutoka kwenye meli kubwa katika gati namba sifuri, huku meli za makasha zikiendelea kuhudumiwa katika magati mengine.

Katibu Mtendaji wa MOESNA, Kassim Mpaata ameahidi kuendelea kuhamasisha matumizi yake. "Tumekuwa tukitumia bandari hii kwa muda mrefu, lakini kwa sasa tumeshuhudia kasi ya juu ya maboresho yanayofanyika hapa," alisema Mpaata.

Hata hivyo, Mpaata aliitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) iendelee na kushughulikia changamoto zinazobainishwa na wadau ili kuongeza ufanisi na

kuvutia wateja zaidi. Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Abdallah Mitawi, aliwashukuru wajumbe 22 waliotembelea kwa kujitoa kwao kuhamasisha matumizi ya bandari hiyo kusafirisha na kupokea bidhaa, zikiwemo mazao ya kilimo na madini.

Maboresho ya kina cha maji kutoka mita 12 hadi mita 14.5 yamewezesha bandari hiyo kupokea meli kubwa zaidi, zenye urefu wa hadi mita 305 na kupelekea ongezeko la shehena tani laki 3 kutoka tani milioni 33.7 mwaka 2025/26 hadi tani milioni 33.4 mwaka 2024/25 ikiashiria kukua kwa shughuli za kibiashara bandarini hapo.

Tanzania yataka sera imara kukabili misukosuko ya uchumi duniani

Tanzania imezitaka nchi wanachama wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia kuimarisha uratibu wa sera za fedha na bajeti ili kudumisha utulivu wa uchumi na kuongeza uwezo wa kukabiliana na misukosuko ya kiuchumi duniani.

Wito huo wa wiki hii ulitolewa na Waziri wa Fedha, Balozzi Khamis Mussa Omar wakati wa mkutano wa kundi la nchi za

Afrika katika IMF uliofanyika pembezoni mwa Mikutano ya Mwaka ya IMF na Benki ya Dunia mjini Bangkok, Thailand.

Balozzi Omar alisema Tanzania imefanyia marekebisho sheria zake ili kuruhusu serikali kuongeza mtaji wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), hatua inayolenga kuimarisha uwezo wa taasisi hiyo kukabiliana na misukosuko ya kiuchumi.

Alitaja vipaumbele vitatu vinavyopaswa

kuzingatwa ili kuimarisha uthabiti wa uchumi ikiwemo kuboresha uratibu wa mtiririko wa fedha za serikali na mipango ya kukopa kwa kuzingatia tathmini za Benki Kuu kuhusu ukwasi katika mfumo wa fedha.

Kipaumbele cha pili ni kuwalinda wananchi na kaya zilizo katika mazingira magumu wakati wa misukosuko ya kiuchumi huku kipaumbele cha tatu kikiwa ni kulinda uwekezaji unaochochea ukuaji wa uchumi.

The Islamic Foundation yasema iko pamoja na serikali 100%

■ Ni katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 mikoa ya Kigoma, Tabora

Uongozi wa Taasisi ya The Islamic Foundation umefanya ziara katika mikoa ya Kigoma na Tabora, ambapo umekutana na viongozi wa Serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi hiyo kwa ajili ya kuboresha huduma za kijamii.

Ziara hiyo, iliyoongozwa na Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Aref Nahdi, imelenga kuimarisha ushirikiano na viongozi wa maeneo husika, kufuatilia utekelezaji wa miradi na kubaini mahitaji mengine ya wananchi yanayoweza kushughulikiwa kwa kushirikiana na Serikali.

Akiwa mkoani Kigoma, Nahdi na ujumbe wake waliitikia mwaliko wa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kigoma, Jamal Tamimi, na kufanya mazungumzo kuhusu namna taasisi hiyo inavyoweza kuongeza mchango wake katika maendeleo ya mkoa.

Mazungumzo hayo yalijikita katika kuimarisha ushirikiano kwenye sekta za elimu, maji na miradi mingine ya kijamii, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuboresha maisha ya wananchi na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Katika mazungumzo hayo, uongozi wa TIF ulieleza dhamira yake ya kuendelea kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali katika kutekeleza miradi inayolenga kupanua upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

Mwenyekiti wa TIF, Aref Nahdi, alisisitiza umuhimu wa kuwekeza katika sekta za elimu na maji, akieleza kuwa huduma hizo zina nafasi kubwa katika kuimarisha ustawi wa jamii na

kujenga msingi wa maendeleo endelevu.

Amesema taasisi hiyo itaendelea kuelekeza nguvu zake katika miradi yenye manufaa kwa wananchi, sambamba na kudumisha ushirikiano na viongozi wa Serikali katika maeneo inakotekeleza shughuli zake.

Wakagua miradi ya maendeleo Kigoma

Mbali na mazungumzo hayo, ujumbe wa TIF ulitembelea shule zinazojengwa na taasisi hiyo pamoja na miradi mingine ya maendeleo mkoani Kigoma, kwa lengo la kujionea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

Ziara hiyo iliwapa viongozi nafasi ya kutathmini maendeleo ya miradi, kubaini mahitaji yaliyopo na kujadili namna ya kuongeza kasi ya utekelezaji ili huduma ziweze kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Katika moja ya maeneo waliyotembelea, viongozi wa eneo hilo waliomba TIF kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita kwenye kiwanja kilichotengwa kwa ajili hiyo.

Ombi hilo lilielezwa kuwa sehemu ya juhudi za kuongeza fursa za elimu kwa vijana wa Kigoma na kuwawezesha kuendelea na masomo ya ngazi za juu bila kukabiliwa na changamoto ya uhaba wa nafasi za shule.

Ujumbe wa TIF ulihusisha pia Mkurugenzi Mtendaji, Sheikh Ibrahim Twaha; Mkurugenzi wa Mkoa wa Dodoma, Arif Saggaf; Mkurugenzi wa Mwanza, Abdu Abeid; na mwenyeji wao, Mkurugenzi wa TIF Mkoa wa Kigoma, Menshi Senga.

Ziara Tabora

Baada ya Kigoma, uongozi huo uliendelea ziara yake mkoani Tabora kwa kutembelea miradi mbalimbali inayosimamiwa na taasisi hiyo, pamoja na maeneo yenye mali za wakfu zilizotolewa na waumini kwa ajili ya kutekelezwa na kunufaisha jamii. Wakiwa Tabora, viongozi hao walipokelewa na Mkurugenzi wa taasisi hiyo Mkoa wa Tabora, Aref Radman, aliyewaongoza katika maeneo mbalimbali na kuwapa maelezo kuhusu miradi inayoendelea na fursa zilizopo za kuendeleza mali za wakfu.



Kutunza bahari iwe ajenda kubwa ya kitaifa

Kuanzia Oktoba 6 hadi 9, 2026, wajumbekutokanchi 10 wanachama wa Mkataba wa Nairobi walikutana katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam kujadili mikakati ya kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na pwani katika ukanda wa Bahari ya Hindi Magharibi.

Mkutano huo wa COP12 ulifanyika wakati Mkataba wa Nairobi ukiadhimisha miaka 40 tangu kuanzishwa kwake.

Miongoni mwa viongozi waliozungumza katika mkutano huo alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hamza Hassan Juma, aliyesema kuwa Tanzania Bara na Zanzibar zina urithi mkubwa wa bahari na pwani unaotoa fursa nyingi za kiuchumi na kijamii.

Waziri Hamza alisisitiza kuwa juhudi za kulinda rasilimali hizo zinapaswa kwenda sambamba na matumizi endelevu ili kuhakikisha zinawanufaisha wananchi wa sasa na vizazi vijavyo. Tunaunga mkono kauli hiyo, kwa kuwa bahari ni chanzo muhimu cha chakula, ajira na mapato kwa mamilioni ya watu.

Hata hivyo, uchafuzi wa bahari, uvuvi haramu na uharibifu wa mifumo ya ikolojia ya baharini vinaendelea kuhatarisha uhai wa rasilimali hizo. Kwa msingi huo,

tunasisitiza kuwa utunzaji wa bahari ni jukumu la pamoja linalohitaji ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi, taasisi za kiraia na jamii za pwani.

Aidha, ni muhimu kutoa elimu kwa umma, kusimamia sheria ipasavyo na kuwekeza katika teknolojia rafiki kwa mazingira ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinahifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu.

Watanzania tujitambue na kuitenda nchi yetu kwa vitendo, ikiwamo kulinda mazingira na rasilimali za bahari ambazo ni sehemu muhimu ya urithi wa taifa.

Uislamu na utunzaji wa bahari

Uislamu unahimiza utunzaji wa mazingira na matumizi sahihi ya rasilimali za asili, ikiwamo bahari, ambazo ni muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine.

Allah anasema: “Wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenezwa kwake, na muombeni kwa hofu na matumaini. Haki-ka rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wafanyao wema.” [Qur’an, 7:56].

Aya hii inatukumbusha wajibu wa kulinda mazingira dhidi ya uharibifu kwa kuepuka kutupa taka baharini, kuharibu makazi ya viumbe na kujihusisha na uvuvi haramu.

Waislamu tunapaswa kuwa

mstari wa mbele katika kutunza mazingira, kwa kuwa dini yetu imetoa dira na mwongozo mahsusi kuhusu wajibu wa binadamu katika kulinda uumbaji wa Allah.

Cha kusikitisha ni kwamba baadhi yetu tumekuwa vinara wa kuharibu mazingira ya bahari, tukisahau kuwa ni rasilimali muhimu inayopaswa kulindwa kwa manufaa ya viumbe vyote. Tabia hii inapingana na wajibu wa binadamu wa kutunza mazingira na kutumia rasilimali kwa uwajibikaji.

Tunapaswa kutambua kwamba kila kilichoumbwa na Allah kina lengo lake ambalo halina budi kutimizwa. Allah anasema: “Hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yake isipokuwa kwa haki na kwa muda maalumu uliokadiriwa...” [Qur’an, 46:3].

Pia anasema: “Na tumekuwekeeni humo vitu vya maisha yenu, na vya hao ambao nyinyi si wenye kuwaruzuku. Na hakuna kitu chochote ila ziko kwetu hazina zake, wala hatukiteremshi ila kwa kipimo maalumu.” [Qur’an, 15:20–21].

Tunachojifunza kutokana na aya hizi ni kwamba vitu vyote vimeumbwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya binadamu na viumbe wengine, kwa mujibu wa hekima na kipimo alichokadiria Allah. Hivyo, hakuna swali juu ya wajibu wa binadamu katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya bahari.

Kenya yapiga hatua kuimarisha Tume ya Waqf

Kenya — Serikali ya Kenya imepiga hatua muhimu katika kuimarisha Tume ya Waqf, baada ya jopo maalumu kukamilisha mchakato wa uteuzi na kupendekeza majina ya watu wanane watakaosimamia mali za Waqf nchini humo.

Mwanasheria Mkuu wa Kenya, Dorcas Odior, amesema jopo hilo limewasilisha ripoti yake ya mwisho pamoja na majina ya walio-pendekezwa kwa ajili ya uteuzi rasmi.

Hatua hiyo inalenga kuiwezesha tume kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Waqf ya mwaka 2022, ikiwa ni pamoja na

kusajili, kusimamia na kulinda mali zilizowe-kwa Waqf kwa manufaa ya jamii.

Kwa mujibu wa taarifa zilizochapishwa na Sahifa Media na The Eastleigh Voice, walio-pendekezwa wanajumuisha mwanazuoni wa Kiislamu, mfanyabiashara na wataalamu sita wenye maarifa na uzoefu katika nyanja mbalimbali.

Mchakato huo ulivutia waombaji 148, ambapo 35 walichaguliwa kwa usaili uliofanyika Septemba 14 hadi 18 mwaka huu.

Jopo hilo limependekeza pia matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kutunza kumbu-

kumbu za mali za Waqf, hati za umiliki, mapato na taarifa za wanufaika ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Hatua hiyo ni ya umuhimu pia kwa Tanzania, ambako kumekuwapo matarajio ya kuanzishwa chombo maalumu cha kitaifa cha kusimamia na kuendeleza mali za Waqf.

Waqf ni utaratibu wa Kiislamu wa kutenga mali kwa manufaa endelevu, ikiwemo kusaidia elimu, afya, misikiti na huduma nyingine za kijamii.

Waliopendekezwana nchini Kenya bado wanasubiri uteuzi rasmi kwa mujibu wa sheria.

Shisha yatajwa kuchochea ongezeko la watoto njiti



Matumizi ya shisha kwa wasichana, hususan wajawazito, yameibua wasiwasi wa kiafya kutokana na athari zake kwa ukuaji wa mtoto tumboni na hatari ya kujifungua mtoto njiti.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Wagonjwa wa Nje wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dkt. Mugisha Nkoronko, alitoa tahadhari hiyo hivi karibuni wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa

vya matibabu kwa ajili ya watoto wanaohitaji uangalizi maalumu hospitalini hapo.

“Kuna uvutaji wa tumbaku kwa njia ya shisha, na wengi wanaovuta ni wasichana. Siku zijazo huenda tukalazimika kuongeza ukubwa wa chumba hiki ili kuhudumia watoto wanaozaliwa na matatizo yanayohusishwa na uvutaji huo,” alisema.

Dkt. Nkoronko alionya kuwa athari za shi-

sha zinaweza pia kuwapata watu wanaovuta moshi wake bila wao wenyewe kutumia bidhaa hiyo, akihimiza jamii kuepuka mazingira yenye moshi huo.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa wanawake kujiandaa kiafya kabla ya kupata ujauzito, kuzingatia lishe bora na kuhakikisha wanapata huduma za afya kwa wakati, ikiwemo kudhibiti upungufu wa damu.

Usimamizi imara, uwazi, ukaguzi tiba ya ubadhirifu Waqf

Waqf wa fedha taslim unaweza kuwa mkombozi wa misikiti, madrasa na huduma za kijamii, lakini bila usimamizi madhubuti, uwazi na ukaguzi, mali hizo ziko hatarini kupotea.

Kuanzishwa kwa kamati za Sharia, kui-marishwa kwa uwazi wa matumizi ya fedha na ukaguzi wa mara kwa mara wa hesabu ni hatua muhimu za kulinda mali za Waqf dhidi ya ubadhirifu na kujenga imani ya wachangiaji katika taasisi za Kiislamu nchini Tanzania.

Hayo yameanishwa na mwanzilishi wa Zaynab Foundation, Salum Awadh, katika semina maalumu kuhusu nafasi, umuhimu na usimamizi wa Waqf wa fedha taslim (cash waqf), iliyofanyika kwa njia ya mtandao, Jumamosi, Oktoba 17, 2026.

Katika wasilisho lake, Awadh alibainisha hatari tano zinazohitaji kudhibitiwa katika usimamizi wa Waqf, ambazo ni kupotea kwa mtaji, mfumuko wa bei, utawala dhaifu au ubadhirifu, kutokuzingatiwa kwa Sharia na kupotea kwa imani ya wachangiaji.

Ili kukabiliana na hatari hizo, aliainisha umuhimu wa kuwepo, Kamati ya Sharia taratibu zinafuatwa. kuwepo ukaguzi wa nje wa hesabu na utoaji wa ripoti kwa wachangiaji kila baada ya miezi mitatu.

Katika kudhibiti hatari za kifedha, semina hiyo imependekeza kutawanya uwekezaji katika maeneo mbalimbali na kurejesha sehemu ya faida kwenye mtaji ili kusaidia kuhifadhi thamani yake dhidi ya mfumuko wa bei.

Nguzo tano za usimamizi

Akifafanua nguzo tano za usimamizi bora wa Waqf ambazo ni utawala, uwekezaji, uzingatiaji wa Sharia, udhibiti wa hatari na uwazi; alisisitiza umuhimu wa hati ya Waqf inayoeleza madhumuni yake, bodi ya wadhamini na msimamizi mwaminifu anayejulikana kama Nadhir au Mutawalli.

Muundo uliopendekezwa katika semina hiyo unahusisha pia meneja wa uwekezaji,

kamati ya Sharia na mkaguzi wa hesabu, huku majukumu yao yakitenganishwa ili kuongeza uwajibikaji.

Aidha, kila mfuko wa Waqf unapaswa kuwa na sera ya uwekezaji iliyoandikwa, inayozingatia uhalali wa Sharia, uwezo wa kulinda mtaji na namna ya kuwafikishia wanufaika mapato yanayopatikana.

Waqf wa fedha taslim ni nini?

Katika semina hiyo, Awadh alieleza Waqf kuwa utaratibu wa kutenga mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, huku asili ya mali hiyo ikihifadhiwa na manufaa yake kuelekezwa kwa walengwa waliokusudiwa; huku akitaja nguzo zake nne kuwa ni mtoaji wa Waqf (Waqif), mali inayowekwa Waqf (Mawquf), walengwa (Mawquf Alayh) na tamko au hati inayobainisha masharti ya Waqf (Sigha).

Alifafanua kuwa tofauti na Waqf wa ardhi au majengo, Waqf wa fedha taslim unamwezesha mtu kuchangia fedha ambazo zinakusanywa katika mfuko na kutumiwa kwa uwekezaji unaokubalika kisharia.

Mapato yatokanayo na uwekezaji huo yanaweza kugharamia shughuli za kijamii, huku usimamizi ukilenga kuhifadhi mtaji wa awali ili manufaa yaendeleo kupatikana.

Semina hiyo imeeleza kuwa hata watu wenye uwezo mdogo wa kifedha wanaweza kushiriki, kwa kuwa michango midogo ya watu wengi inaweza kujenga mfuko mkubwa wa Waqf.

Misingi yake katika Uislamu

Akizungumzia msingi wa Waqf, Awadh alirejea Qur'an, [3:92], inayohimiza kutoa katika mali zinazopendwa. "Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua."

Ameeleza pia Hadith inayohusu Umar bin Al-Khattab, ambaye Mtume Muham-mad (Allah amshushie rehema na amani) alimuelekeza kuhifadhi asili ya ardhi yake ya Khaybar na kutoa manufaa yake katika sadaka.

Vilevile, amerejea Hadith ya Sahih Muslim inayotaja sadaka yenye kuendelea kuwa miongoni mwa amali zinazomnufaisha mtu baada ya kufariki.

Kuhusu uhalali wa Waqf wa fedha, wasilisho limetaja Azimio Namba 140 (15/6) la mwaka 2004 la Baraza la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu (International Islamic Fiqh Academy - IIFA), linalotambua Waqf wa fedha kwa kuzingatia uhifadhi wa mtaji na matumizi yanayokubalika kisharia.

Njia za kutumia Waqf

Semina hiyo imeainisha njia mbalimbali za kutumia Waqf wa fedha, ikiwemo kuanzisha mifuko ya uwekezaji, kutoa mikopo isiyo na riba (Qard Hasan), kuchangisha michango kupitia vipande vya Waqf na kuwekeza katika hati fungani za Kiislamu (sukuk).


Mapato ya Waqf yanaweza kusaidia uendeshaji na matengenezo ya misikiti, misha-hara ya walimu wa madrasa na maimamu, elimu ya wanafunzi wasiojiweza na huduma za afya.

Aidha, yanaweza kusaidia miradi ya uweze-shaji wa wanawake na vijana pamoja na kutoa msaada wakati wa maafa.

Kwa mujibu wa Zaynab Foundation, mfu-mo huo unaweza kusaidia taasisi za Kiislamu kupunguza utegemezi wa michango ya kila mara kwa kujenga vyanzo endelevu vya mapato.

Hata hivyo, semina imesisitiza kwamba mafanikio ya Waqf wa fedha yanategemea usimamizi makini, uwekezaji halali na uwezo wa kudhibiti hatari zinazoweza kusababisha hasara.

Zaynab Foundation imesema iko tayari kushirikiana na misikiti, madrasa na taasisi za Kiislamu katika kutoa elimu, kubuni mifumo na kuanzisha miradi ya Waqf wa fedha taslim.



Ebola yatishia Kenya, Tanzania tahadhari juu

Tanzania imeimarisha uchunguzi wa afya katika mipaka yake kufuatia kuongezeka kwa wagonjwa wa Ebola nchini Kenya hadi kufikia saba, akiwemo mmoja aliyefariki dunia, huku mlipuko mkubwa wa ugonjwa huo ukiendelea kusambaa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Hatua hiyo imefuatia uthibitisho wa wagonjwa wengine wanne nchini Kenya, Jumamosi, Oktoba 17, 2026, wakiwemo wahudumu wata-tu wa afya na ndugu wa mgonjwa wa kwanza aliyefariki Oktoba 5.

Wizara ya Afya ya Kenya imesema wahu-dumu hao ni wanaume wawili wenye umri wa miaka 29 na 35 na mwanamke mwenye miaka 32, waliomhudumia mgonjwa wa kwanza kati ya Oktoba 3 na 4.

Wagonjwa hao walikuwa tayari katika karantini walipoanza kuonyesha dalili na kut-hibitishwa kuwa na virusi vya Ebola vya aina ya Bundibugyo.

Serikali ya Kenya imesema watu 128 kati ya 130 waliotambuliwa kuwa walikutana na

mgonjwa wa kwanza wamepatikana na kuwe-kwa karantini, huku wawili wakiendelea kuta-futwa.

Licha ya kugundulika kwa maambukizi kati ya watu waliokutana na mgonjwa wa kwanza, mamlaka za Kenya zimesema hakuna usha-hidi wa maambukizi yanayoenea katika jamii kwa ujumla.

Tanzania yaimarisha tahadhari

Kufuatia hali hiyo, Wizara ya Afya ya Tan-zania imetoa Mwongozo wa Tahadhari kwa Wasafiri Na. 18 wa Oktoba 17, 2026, unaolenga kuzuia kuingia kwa ugonjwa huo nchini.

Kwa mujibu wa mwongozo uliosainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Maghembe, wasafiri wote wanaoingia Tanza-nia wanatakiwa kujaza fomu za taarifa za afya kwa njia ya mtandao na kufanyiwa uchunguzi katika maeneo ya kuingilia nchini.

Uchunguzi huo unahusisha upimaji wa joto la mwili, huku wasafiri wanaotambuliwa kuwa

katika hatari kubwa ya maambukizi wakifua-tiliwa kwa siku 21.

DRC yafikisha vifo 4,536

Wakati huo huo, mlipuko wa Ebola nchi-ni DRC umeenea hadi jimbo la nane, North Ubangi, ambako wagonjwa wawili wamethibi-tishwa, akiwemo mmoja aliyefariki.

Kwa mujibu wa Reuters, DRC ilikuwa imer-ekodi wagonjwa 9,415 na vifo 4,536 kufikia Oktoba 16, 2026. Mlipuko huo ulioanza Mei mwaka huu umeenea pia nje ya DRC, ikiwemo Kenya. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Ebola huambukizwa kupitia kugu-sana moja kwa moja na damu au majimaji ya mwili wa mtu mwenye maambukizi, pamoja na vifaa vilivyochafuliwa na majimaji hayo.

Dalili zake ni homa, uchovu, maumivu ya kichwa na misuli, kutapika na kuharisha.

WHO inasisitiza umuhimu wa kutambua wagonjwa mapema, kuwapatia huduma, kuwafuatilia waliokutana nao na kuimarisha udhibiti wa maambukizi.

Watoto 340 wauawa Gaza licha ya sitisho la vita



Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) limeripoti kuwa zaidi ya watoto 340 wameuawa katika Ukanda wa Gaza tangu kutangazwa kwa makubaliano ya kusitisha vita mwaka 2025, huku wengine takribani 800,000 wakiendelea kuishi katika mazingira hatarishi baada ya kulazimika kuyakimbia makazi yao kutokana na mashambulizi ya Israel.

Kwa mujibu wa UNICEF, takribani watoto 60,000 wamepoteza mzazi mmoja au wote

wawili kutokana na vita hivyo, wakati maelfu ya familia zikiendelea kuishi katika mahema yaliyochakaa na majengo yaliyoharibiwa. Hali hiyo inazidi kuwa mbaya wakati msimu wa baridi ukikaribia, huku watoto wengi wakihitaji msaada wa kisaikolojia.

Hata hivyo, shirika hilo limesema juhudi za kibinadamu zimewezeshwa zaidi ya watoto 560,000 kurejea katika shughuli za kuji-funza, huku watu milioni 1.2 wakipatiwa maji salama. Pamoja na hatua hizo, mitambo

yote sita ya kusafisha majitaka bado haifanyi kazi, hali inayoongeza hatari ya magonjwa na mafuriko. UNICEF imeitaka jumuiya ya kimataifa kuhakikisha makubaliano ya kusitisha vita yanatekelezwa kikamilifu, misaada inaruhusiwa kuingia bila vikwazo na huduma muhimu zinarejeshwa. Shirika hilo limesisitiza kuwa amani ya kweli kwa watoto wa Gaza inapaswa kupimwa kwa usalama wao, upatikanaji wa elimu na haki yao ya kuishi maisha ya kawaida.



Trump akera Waislamu kwa mzaha kuhusu jina Muhammad

Rais wa Marekani, Donald Trump, amezua mjadala baada ya kufanya mzaha kuhusu jina la Muhammad, linaloheshimiwa na kutumiwa kwa wingi na Waislamu duniani kwa heshima ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani.).

Akizungumza katika mkutano wa kampe-ni jimboni Georgia, Ijumaa, Oktoba 16, 2026, Trump alisema kwamba mtu asipokuwa na

uhakika wa jina la mtu kutoka Mashariki ya Kati, anaweza kumwita Muhammad na kuwa na uwezekano wa asilimia 65 wa kupatia.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Trump alidai amekuwa akitumia mbinu hiyo kwa miaka mingi bila kukosea.

Reuters imeripoti kwamba mzaha huo haukupokelewa kwa shangwe kubwa na waliohudhuria mkutano huo. Tukio hilo limeangaziwa

pia na Al Jazeera pamoja na vyombo vingine vya habari vya kimataifa.

Mashirika ya kutetea haki za Waislamu nchini Marekani yamekuwa yakimkosoa Trump kwa kauli wanazosema zinachochea chuki na ubaguzi dhidi ya Waislamu.

Mapema mwaka huu, Baraza la Mahusiano ya Marekani na Uislamu (CAIR) lilihusisha ongezeko la chuki dhidi ya Waislamu na baadhi

Mataifa 19 yailaani Colombia kusimika ubalozi Jerusalem

Mawaziri wa Mambo ya Nje wa mataifa 19, yakiwemo Saudi Arabia, Uturuki, Pakistan, Indonesia na Malaysia, wamelaani hatua ya Colombia kuwa taifa la 10 kufungua ubalozi wake mjini Jerusalem Oktoba 14, wakisema uamuzi huo unakiuka maazimio ya Umoja wa Mataifa na kutishia juhudi za kuanzishwa kwa taifa huru la Palestina.

Katika tamko la pamoja lililotolewa Oktoba mwishoni mwa wiki hii, mawaziri hao wamesema hatua ya Colombia inapingana na maazimio namba 476 na 478 ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ya mwaka 1980, yanayopinga hatua za kubadilisha hadhi ya kishe-ria na kihistoria ya Jerusalem. Wamesisitiza kuwa Jerusalem Mashariki inapaswa kuwa mji mkuu wa taifa huru la Palestina.

Uamuzi huo umefanywa na Rais Abelardo de la Espriella, aliyerejesha uhusiano wa

kidiplomasia na Israel baada ya mtangulizi wake kuuvunja mwaka 2024 kutokana na vita vya Gaza.

Mataifa yaliyotia saini tamko hilo yamesisitiza kuwa hatua za upande mmoja kuhusu Jerusalem haziwezi kuondoa haki za Wapalestina zinazotambuliwa na sheria za kimataifa na kuitaka Colombia itengue uamuzi wake na kuheshimu juhudi za kimataifa za kufikia suluhisho la mataifa mawili.

Chanzo: Reuters & Anadolu Ajensi

Mataifa 57 ya Kiislamu kukutana kujadili migogoro ya Dunia

Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) imeandaa mkutano wake wa 52 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje mjini Baghdad, Iraq, unaotarajiwa kufanyika Oktoba 17 na 18, 2026, ukilenga kuimarisha mshikamano wa nchi wanachama 57 katika kukabiliana na migogoro ya kisiasa, changamoto za kibi-

nadamu na mahitaji ya maendeleo katika ulimwengu wa Kiislamu.

Katibu Mkuu wa OIC, Ismail Ould Cheikh Ahmed, amewasili Baghdad akiongoza ujumbe wa ngazi ya juu wa jumuiya hiyo. Mkutano huo unaongozwa na kaulimbiu inayosisitiza mazungumzo na mshikamano kama nguzo muhimu za kuimarisha amani na maendeleo endelevu.

Miongoni mwa masuala yanayotarajiwa kujadiliwa ni hali ya Palestina, migogoro ya Sudan, Yemen na Afghanistan, pamoja na hatua za kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na usalama wa chakula.

Jumuiya hiyo pia inatarajiwa kupitia changamoto zinazozikabili jamii za Waislamu katika maeneo mbalimbali duniani na taarifa yake ya mwaka 2025 kuhusu chuki dhidi ya Uislamu.

Kwa upande wa Afghanistan, mjadala unatarajiwa kugusa pia mahitaji ya kibinadamu na hali ya elimu, kufuatia juhudi za mjumbe maalumu wa OIC, Dkt. Tarig Ali Bakheet, kuitaka serikali ya Taliban kuwezesha wasichana kupata elimu, ikiwemo mafunzo ya udaktari na afya

Chanzo: Kabul News

Ufaransa yatikiswa kwa maandamano makubwa



Rais Emmanuel Macron anakabiliwa na shinikizo kubwa la kisiasa baada ya mamia ya maelfu ya wananchi kuandamana nchini Ufaransa kupinga kupanda kwa gharama za maisha, hali mbaya ya elimu na huduma za umma, huku vurugu zikisababisha kukamatwa kwa zaidi ya watu 2,000.

Maandamano hayo ya Jumamosi, Oktoba 17, 2026, yalianza kama muendelezo wa malalamiko ya wanafunzi wa shule za sekondari yaliyoibuka Septemba, wakipinga uhaba wa walimu, uchakavu wa shule na mazingira magumu ya kujifunzia.

Baadaye, vyama vya wafanyakazi, wanafunzi wa vyuo na makundi mengine yaliungana nao kupinga kupanda kwa bei za chakula, mafuta na nishati, mishahara isiyokidhi mahitaji na

gharama kubwa za maisha.

Kwa mujibu wa mamlaka za Ufaransa, waandamanaji wapatao 550,000 walishiriki, huku vyama vya wafanyakazi vikikadiria idadi hiyo kufikia 800,000.

Ingawa maandamano mengi yalikuwa ya amani, vurugu zilizuka katika miji ya Paris, Marseille, Lyon na Limoges, ambako majengo ya serikali na biashara yalivamiwa, kuchomwa moto au kuporwa.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Laurent Nuñez, amesema zaidi ya watu 2,000 walikamatwa, huku zaidi ya polisi na wazima moto 600 waki- jeruhiwa.

Akilihutubia taifa Jumapili, Oktoba 18, Macron alikiri umuhimu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi lakini akaonya

kwamba wahusika wa uharibifu watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema Waziri Mkuu Sébastien Lecornu ataongoza timu ya kushughulikia athari za vurugu na changamoto zilizojitokeza.

Serikali tayari imeahidi kuongeza walimu wa muda na kuachana na mpango wa kuongeza ada za vyuo vikuu, lakini waandamanaji wanataka hatua pana zaidi za kupunguza gharama za maisha.

Mgogoro huo umeongeza shinikizo kwa serikali kabla ya uchaguzi wa rais unaotarajiwa kufanyika mwaka 2027.

Mustakabali wake utategemea uwezo wa serikali kushughulikia madai ya wananchi, kurejesha utulivu na kufikia makubaliano na vyama vya wafanyakazi na wanafunzi.



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Je, mume anamrithi mke wake aliyemtaliki akifariki kabla ya kumaliza eda?

Swali: Mwanamume alimuoa mwanamke, kisha akamtaliki talaka ya kwanza. Mwanamke huyo alipokuwa bado katika eda, alifariki dunia. Je, mume huyo ana haki ya kurithi mali aliyoiacha mwanamke huyo?

Jibu: Mwanamke akifariki dunia kabla ya kumaliza eda ya talaka rejea, mume wake humrithi kwa makubaliano ya wanazuoni wa Kiislamu.

Hii ni kwa sababu mwanamke huyo bado huhukumiwa kuwa katika hali ya ndoa maadamu yuko ndani ya eda ya talaka rejea. Vivyo hivyo, mume akifariki katika kipindi hicho, mwanamke huyo humrithi.

Ama ikiwatalakaniyakubainisha (twalaq bain), wanandoa hawarithiani katika hali ya kawaida. Hali hii inajumuisha mifano ifuatayo:

Kwanza, talaka ya fidia (Khul'): Mwanamke anapompa mumewe fidia ili amtaliki, kisha akamwacha kwa talaka ya aina hiyo.

Pili, Khul' bila kutumia tamko la talaka: Mume anapokubali kuvunja ndoa kwa fidia ya mwanamke kwa kutumia tamko la khul' badala ya tamko la talaka.

Tatu, kuvunjwa kwa ndoa na kadhi au hakim: Ndoa inapofasakhiwa kwa sababu inayokubalika kisharia.

Nne, Talaka ya tatu: Mwanamume anapompa mkewe talaka ya tatu, bila kuwa anatumia kuwa amefanya hivyo kwa nia ya

kumnyima haki ya urithi.

Katika hali hizo nne, utengano huwa ni wa kubainisha (baynunah), na kwa hukumu iliyotajwa katika fatwa hii, wanandoa hawarithiani. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

Wasio Waislamu wanamrithi Muislamu?

Swali: Mke wangu amefariki dunia. Ameacha watoto watatu: binti mmoja na wavulana wawili, pamoja na mume (mimi), dada zake watatu Wanaswara, ndugu zake wawili ambapo mmoja ni Mnaswara, na baba pamoja na mama ambao pia si Waislamu. Je, urithi wake utagawanywa vipi, na kila mmoja atapata sehemu gani?

Jibu: Ikiwa marehemu alikuwa Muislamu, basi hawamrithi isipokuwa warithi wake walio Waislamu.

Watu wasiokuwa Waislamu hawamrithi Muislamu, kwa mujibu wa hadithi ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Muislamu hamrithi kafiri, wala kafiri hamrithi Muislamu." [Bukhari, Na. 6764, na Muslim, Na. 1614].

Sheikhul-Islam Ibn Taymiyyah amesema: "Waislamu wamekubaliana kuwa kafiri hamrithi Muislamu, wala kafiri haoi mwanamke Muislamu." [Al-Fatawa Al-Kubra, 3/130].

Kwa msingi huo, urithi wa mwanamke huyo utagawanywa kama ifuatavyo: Mume: Atapata robo (1/4), kwa sababu marehemu amechacha watoto. Mwenyezi Mungu amesema: "Ikiwa wake zenu wana mtoto, basi nyinyi mtapata robo ya walichokiacha baada ya kutekelezwa wasia waliouusia au kulipwa deni." [Qur'an, 4: 12].

Watoto watatu: Binti mmoja na wavulana wawili watagawana mali iliyobaki kwa kanuni ya kwamba mwanaume hupata sehemu mara mbili ya mwanamke, kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu: "Mwenyezi Mungu anakuusieni kuhusu watoto wenu: mwanaume apate sehemu iliyo sawa na sehemu ya wanawake wawili." [Qur'an, 4: 11].

Ndugu wa marehemu hawapati chochote. Hata ndugu yake ambaye ni Muislamu harithi kwa sababu amezuiliwa na uwepo wa watoto wa kiume.

Baba na mama wasio Waislamu hawarithi, kwa sababu tofauti ya dini huzuia urithi kati ya Muislamu na asiye Muislamu.

Ikiwa marehemu hakuwa Muislamu:

Iwapo mwanamke aliyefariki hakuwa Muislamu, basi kwa hukumu iliyotajwa katika fatwa hii, watakaomrithi ni wale walio katika dini yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

Hoja ni ileile hadithi ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliposema: "Muislamu hamrithi kafiri, wala kafiri hamrithi Muislamu." [Bukhari, Na. 6764, na Muslim, Na. 1614].



Haki na wajibu wa mke aliye katika eda

Katika makala iliyopita, tuliangazia maana ya eda kwa mujibu wa Sharia, wajibu wa mwanamke kukaa eda na hekima iliyomo katika agizo hilo. Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, tutaeleza aina nane za eda kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.

Haki na wajibu wa mke aliye katika eda

Mosi, eda ya mjamzito

Eda ya mwanamke mjamzito huisha mara tu anapojifungua, hata kama amejifungua muda mfupi tu baada ya kufiwa na mumewe au kupewa talaka. Hukumu hii inatokana na kauli ya Allah Mtukufu: "...Na wanawake wenye mimba, muda wao wa eda ni mpaka wajifungue..." [Qur'an 65:4].

Pili, eda ya aliyefiwa na mume akiwa si mjamzito

Mwanamke aliyefiwa na mume akiwa si mjamzito atakaa eda miezi minne na siku 10. Hukumu hii inatokana na kauli ya Allah Mtukufu: "Na wale wanaokufa miongoni mweni na wakaacha wake, hao wake wangoje peke yao (kwa kukaa eda) miezi minne na siku kumi..." [Qur'an, 2:234].

Tatu, eda ya mwanamke ambaye bado anapata hedhi

Mwanamke aliyepewa talaka na ambaye bado anapata hedhi hukaa eda kwa kuhesabu hedhi tatu, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu: "Na wanawake walioachwa wangoje peke yao mpaka twahara (au hedhi) tatu zipite..." [Qur'an, 2:228].

Nne, eda ya aliyekoma hedhi

Mwanamke aliyekoma hedhi hukaa eda kwa miezi mitatu, kwa kauli ya Allah Mtukufu: "Na wale waliokoma hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mna shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi. Na wenye mimba eda yao mpaka watakapozaa..." [Qur'an, 65:4].

Tano, eda ya aliyekatika hedhi bila sababu

Mwanamke ambaye hedhi yake imekatika bila kujua sababu, huku akiwa hajafikia umri wa kukoma hedhi, hukaa eda kwa muda wa mwaka mmoja kamili.

Kwa mujibu wa maelezo haya ya kifikihi, miezi tisa ya kipindi hicho huhesabiwa kwa ajili ya kubaini iwapo mwanamke huyo ana ujauzito, huku miezi mitatu iliyobaki ikiwa ni muda wa eda unaohusishwa na kukoma kwa hedhi.

Hata hivyo, ikiwa mwanamke huyo atapata hedhi katika kipindi hicho, hata kwa muda mfupi, atakaa eda kwa utaratibu unaotumika kwa mwanamke anayepata hedhi. Aidha, ikiwa itajulikana kuwa kukatika kwa hedhi kumesababishwa na hali fulani, kama vile ugonjwa au kunyonyesha, atakaa eda hadi hedhi yake itakaporudi.

Imam Shafi'i (Allah amrehemu) amesema kuwa huo ndio uamuzi uliofanywa na Khalifa Umar bin Khattwab (Allah amridhie) mbele ya Muhajirun na Answar, na hakuna aliyepinga uamuzi huo. Hivyo, unachukuliwa kuwa ni makubaliano ya pamoja.

Sita, eda ya mwanamke aliyezini

Kuhusu mwanamke aliyechumbiwa ambaye anadaiwa kuwa huenda alifanya kitendo cha zinaa, baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa, katika suala la istibra (kipindi cha kusubiri ili kubaini kama ana ujauzito) hupewa muda wa hedhi moja ili kuhakikisha kuwa hana ujauzito wa mwanaume mwingine.

Aidha, wanazuoni wote wamekubaliana kuwa mwanamke aliyefiwa na mumewe katika ndoa sahihi ana wajibu wa kuomboleza katika kipindi cha eda, hata kama hakuwahi kufanya tendo la ndoa na mume huyo.

Mtume (rehehema Allah na amanizimshukie) amesema: "Si halali kwa mwanamke anayemwamini Allah na Siku ya Mwisho kumuombolezea maiti zaidi ya siku tatu, isipokuwa amkalie

mumewe (eda) miezi minne na siku kumi." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii inaonesha kuwa mwanamke aliyefiwa na mumewe ana wajibu wa kuomboleza katika kipindi chote cha eda. Katika kipindi hicho, anaruhusiwa kutoka mchana ili kutafuta mahitaji ya msingi na ya lazima ambayo hana budi kuyapata, hasa ikiwa hakuna mtu wa kumsaidia kuyapata.

Wanazuoni wa madhehebu wa Maliki wamesema kuwa mwanamke aliye katika eda anaruhusiwa kuhudhuria harusi, lakini haruhusiwi kujipamba wala kuvaa mavazi ya kujionyesha au yanayokusudiwa kwa ajili ya urembo.

Kadhalika, wanazuoni wote wamekubaliana kuwa mwanamke aliye katika eda ya kufiwa na mume anaruhusiwa kuvaa nguo yoyote inayotambulika katika jamii kuwa si ya urembo, bila kujali rangi yake. Pia, anaruhusiwa kujisafisha na kujitunza kwa kiwango kinachokubalika, bila kujipamba kwa lengo la kuwavutia wanaume. Wanazuoni wamekubaliana kuwa hairuhusiwi kumposa moja kwa moja mwanamke aliye katika eda ya kufiwa na mumewe, isipokuwa kwa njia ya ishara. Aidha, wameeleza kuwa ni haramu kumposa mwanamke aliye katika eda kwa kauli ya wazi. Vilevile, hairuhusiwi kuanzisha mazungumzo ya kimapenzi naye wala kumshawishi kufunga ndoa.

Hii ni kwa sababu ombi la wazi la uchumba linaweza kumfanya aharakishe kumaliza eda yake au hata kusema uongo kuhusu kumalizika kwake. Hivyo, kitendo hicho kimekatazwa kisharia kwa lengo la kulinda haki zinazohusiana na eda na kuzuia udanganyifu.

Kuashiria ni kutoa kauli kama: "Ninafahamu ukoo wako, wewe ni mwanamke mwema na nina nia ya kukuo", au kusema, "Mimi niko peke yangu", pamoja na maneno mengine yanayoonesha nia ya ndoa bila kutamka wazi ombi la uchumba.

Saba, eda ya aliyepotelewa na mume na aliyeomba khul'u

Mwanamke aliyepotelewa na mume, bila kujulikana kama yuko hai au amefariki, muda wa eda yake huamuliwa na Kadhi (Hakimu). Kwa upande mwingine, mwanamke aliyeomba khul'u (kuachana na mume kwa fidia) hukaa eda kwa muda wa hedhi moja.



Afyais natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED

P.O. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe 11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email: info@watercomtz.com



HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

NA

**Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383**



Fedha za Kiislamu zapigiwa chapuo kuwa nyenzo ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea

JAKARTA, Indonesia — Mfumo wa fedha za Kiislamu umetajwa kuwa na uwezo wa kusaidia nchi zinazoendelea kupata vyanzo mbadala vya kugharamia miradi ya maendeleo, kupunguza utegemezi wa mikopo na kupanua fursa za kiuchumi kwa wananchi.

Hoja hiyo imetolewa na Hari Suciono, mtaalamu wa uchumi katika Benki Kuu ya Indonesia, kupitia makala yake iliyochapishwa Oktoba 15, 2026, kwenye tovuti ya

Eurasia Review, yenye kichwa Can Islamic Finance Become the Global South's Alternative Development Model?

Suciono amesema nchi zinazoendelea zinakabiliwa na changamoto za madeni, upungufu wa fedha za maendeleo na mahitaji makubwa ya uwekezaji katika miundombinu, chakula, nishati na huduma za kijamii.

Kwa mujibu wake, sekta ya fedha za Kiislamu duniani sasa ina mali zinazozidi dola

trilioni nne za Marekani, huku thamani ya sukuk zilizopo sokoni ikizidi dola trilioni moja. Alieleza kuwa mfumo huo, unaoisitiza uwekezaji katika shughuli halisi za kiuchumi na ugawaji wa hatari, unaweza kusaidia kugharamia miundombinu, nishati jadidifu na biashara ndogo na za kati.

Aidha, alisema taasisi za zakat na wakfu zinaweza kuunganishwa na mifumo ya kifedha ya kibiashara ili kuongeza manufaa ya kijamii.

Zakat, wakfu ni fursa za mitaji kwa wafanya-biashara wadogo



JAKARTA, Indonesia — Indonesia inaendeleza mfumo wa kuunganisha fedha za zakat na wakfu na huduma za benki za Kiislamu ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo kupata mitaji, kukuza biashara na kujikwamua kiuchumi.

Katika makala iliyochapishwa Oktoba 15, 2026 kwenye tovuti ya Eurasia Review, mchambuzi wa uchumi wa Benki Kuu ya Indonesia, Rabiul Misa, amesema mfumo huo unalenga kusaidia biashara ambazo zinashindwa kupata mikopo kutokana na ukosefu wa dhamana au historia ya kifedha inayokubalika benki.

Alieleza kwamba fedha za kijamii za Kiislamu zinaweza kusaidia kugharamia mafunzo, kupunguza gharama za mitaji na kufidia sehemu ya hasara za awali katika mifumo inayoruhusiwa kisharia.

Hatua hiyo inaweza kuwawezesha wajasiriamali kujenga biashara imara kabla ya kuhamia kwenye huduma za kawaida za ufadhili wa benki za Kiislamu.

Hata hivyo, aliongeza kwamba mafanikio ya mfumo huo yatategemea usimamizi wa fedha za zakat na wakfu kwa kuzingatia masharti yake ya kisharia, uwazi na matokeo halisi kwa wajasiriamali.

Mtazamo huo unatoa funzo kwa nchi zinazoendelea kuhusu namna fedha za kijamii za Kiislamu zinavyoweza kusaidia maendeleo ya biashara na kupunguza umaskini.

Benki Kuu ya Somalia yajiunga na AAOIFI

MANAMA, Bahrain — Benki Kuu ya Somalia (CBS) imejiunga na Shirika la Uhasibu na Ukaguzi kwa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI), hatua inayolenga kuimarisha usimamizi, uwazi na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa katika sekta ya fedha za Kiislamu nchini humo.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Somalia (SONNA), uanachama huo uliidhinishwa wakati wa Mkutano wa 24 wa Mwaka wa Bodi

za Sharia za AAOIFI, uliofanyika Manama, Bahrain.

Benki Kuu ya Somalia iliwakilishwa katika mkutano huo na Naibu Gavana wake, Dkt. Ali Yassin.

Hatua hiyo inaiwezesha Somalia kuimarisha ushirikiano na taasisi mbili muhimu za kimataifa zinazoweka viwango vya fedha za Kiislamu, baada ya kuwa tayari mwana-chama wa Bodi ya Huduma za Fedha za Kiislamu (IFSB).

AAOIFI huandaa viwango vya Sharia, uhasibu, ukaguzi na utawala kwa taasisi za fedha za Kiislamu.

Uanachama huo unatarajiwa kusaidia juhudi za Somalia kuboresha kanuni za usimamizi wa benki, kuimarisha uwajibikaji na kukuza sekta ya fedha za Kiislamu inayozingatia viwango vinavyotambulika kimataifa.



NGUVU YA WAQF:

Yadhamini vijana 25 Ibun Jazar Islamic Schools kujiunga na Albukhari International University

Leo tunachambua kwa kina mfumo wa Waqf na jinsi unavyoweza kubadilisha maisha ya Watanzania, tukirejea udhamini wa vijana 25 kwenda masomoni nje ya nchi.

Huu ni mlinganyo wa umma unaotaka kusi-mama: Wahyi unaotoka kwa mahafidh wa Qur'an kutoka kituo cha Ibn Jazar na elimu inayokwenda kutafutwa ugenini katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Albukhary (AIU) nchini Malaysia.

Jinsi mfumo wa Waqf unavyofanya kazi

Mzunguko wa kudumu wa fedha na endelevu wa Waqf unajengwa kupitia utoaji wa mtaji wa awali kama waqf wa milele, uwekezaji halali kwenye biashara au miundombinu, uzalishaji wa faida inayofadhili elimu, na uendelevu wa milele wa vizazi hadi vizazi.

Taasisi ya Albukhary inamiliki mali kubwa zilizowekwa kama Waqf nchini Malaysia, zikiwemo Jumba la Makumbusho ya Sanaa ya Kiislamu, majengo ya ghorofa, na vituo

vya ununuzi. Mali hizi zinazalisha mapato endelevu kupitia ukodishaji na biashara mbalimbali.

Mbali na Waqf, taasisi pia huongezea fedha za Zakat kutoka kwa kampuni zake na wakati mwingine mchango wa kibinafsi kutoka kwa utajiri wa mwanahisani Tan Sri Syed Mokhtar Albukhary, huku Waqf ikiwa ndio uti wa mgongo na chanzo cha uhakika cha milele.

Kuhusu Tan Sri Syed Mokhtar Albukhary, huyu ni mmoja wa wafanyabiashara na wafadhili mashuhuri nchini Malaysia, ambaye licha ya kuanza maisha kwa unyonge na kushindwa kumaliza shule ya upili, amejenga himaya kubwa ya kibiashara inayojumuisha sekta za usafirishaji, magari, na miundombinu.

Kupitia taasisi aliyoiasisi ya Albukhary (Albukhary Foundation), amejitolea kwa hali na mali kusaia jamii ambapo katika sekta ya elimu, amefanya mapinduzi makubwa kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Albukhary (AIU) kinachotoa ufadhili kamili wa masomo (scholarships) kwa wanafunzi wasiojiweza kutoka mataifa zaidi ya 40 duniani, akiamini kuwa elimu ndiyo silaha kuu ya kujikwamua kutoka kwenye umaskini.

Nyayo za kihistoria: vyuo vikuu vya awali vilivyojengwa kwa Waqf

Ili kuelewa nguvu ya mfumo usioweza kuingiliwa na siasa, ni muhimu kuangalia vyuo vikuu vya kihistoria vya Kiislamu vilivyoendeshwa kabisa na Waqf:

Hii hapa orodha iliopanuliwa zaidi kwa kuongeza vyuo vikuu na madrasah nyingine maarufu za kihistoria ambazo nazo zilianzishwa au kuendeshwa kwa mfumo wa Waqf, pamoja na kutoa maelezo yaliyopanuka kwa kina zaidi:

Mosi, Chuo Kikuu cha Ez-Zitouna – Tunisia

Chuo hiki kilianzishwa karibu mwaka 737 Miladia (karne ya nane) mjini Tunis, Tunisia, wakati wa Dola ya Umayyad, kwa mchango wa viongozi wa eneo hilo Mali na ardhi zilizotolewa kama waqf zilitumika kugharamia walimu, uendeshaji wa msikiti na chuo, pamoja na huduma kwa wanafunzi.

Ez-Zitouna ni miongoni mwa vyuo vikuu vya zamani zaidi duniani na kituo kikubwa cha elimu ya Kiislamu na sayansi Afrika Kaskazini. Miongoni mwa wahitimu wake maarufu ni mwanahistoria Ibn Khaldun.

Pili, Chuo Kikuu cha Al-Qarawiyyin – Morocco

Chuo hiki kilianzishwa mwaka 859 Miladia katika mji wa Fez, Morocco, na Fatima al-Fihri. Kwa mujibu wa maelezo yaliyowasilishwa, Fatima al-Fihri alitenga urithi wake wote kama waqf kwa ajili ya kuendesha taasisi hiyo, kujenga nyumba za walimu na kutoa elimu bila malipo.

Chuo hicho kinatambuliwa na UNESCO na Guinness World Records kama mojawapo ya taasisi kongwe zaidi za elimu ya juu duniani zinazoendelea kufanya kazi bila kukatika tangu kuanzishwa kwake. Tukio la vijana wa Ibn Jazar linakumbusha historia ya Fatima al-Fihri, ambaye alitumia urithi wake wote kama Waqf kwa ajili ya kuanzisha taasisi ya elimu.

Tatu, Chuo Kikuu cha Al-Azhar – Misri

Chuo cha Al-Azhar kilianzishwa mwaka 975 Miladia mjini Cairo, Misri, chini ya utawala wa Usultani wa Fatimid. Mali kubwa za waqf, zikiwamo ardhi za kilimo na masoko, zilitumika kugharamia elimu, chakula, posho za wanafunzi na mishahara ya walimu.

Al-Azhar kilikuwa kituo kikuu cha taaluma za Kiislamu na sayansi katika ulimwengu wa Kiarabu. Kimeendelea kuwa na ushawishi mkubwa wa kisomo duniani.

Nne, Madrasah ya Sankore – Mali

Madrasah ya Sankore, inayojulikana pia kama Sankore University, ilianzishwa katika mji wa Timbuktu, Mali, katika karne ya 10, ingawa ilistawi zaidi kati ya karne ya 14 na 16. Taasisi hiyo ilianzishwa na kuendelezwa kwa

NGUVU YA WAQF:

juhudi za jamii ya eneo hilo, wafanyabiashara matajiri na viongozi mbalimbali, akiwamo Mansa Musa. Mali za waqf zilizotolewa na wafanyabiashara matajiri zilihakikisha upatikanaji wa maktaba kubwa, mishahara ya walimu na chakula cha bure kwa wanafunzi. Sankore ilikuwa kituo kikubwa cha elimu ya juu Afrika Magharibi, kilichohifadhi maelfu ya maandishi ya sayansi, hesabu, sheria na elimu ya dini. Kilikuwa na uwezo wa kuku-sanya wanafunzi na wanazuoni kutoka mae-neo mbalimbali.

Tano, Madrasah ya Al-Nizamiyya – Iraq

Madrasah ya Al-Nizamiyya ilianzishwa mwaka 1065 Miladia mjini Baghdad, Iraq, na Nizam al-Mulk, aliyekuwa Waziri wa Dola ya Seljuk. Taasisi hiyo ilifadhiliwa kikamilifu kupitia mfumo wa waqf wa serikali, uliotoa elimu, malazi na ruzuku za kifedha kwa wanafunzi bila malipo.

Al-Nizamiyya iliweka misingi ya mfumo wa mtandao wa kwanza wa vyuo vikuu vinavyotambulika rasmi na serikali, vyenye mitaala na utaratibu uliopangwa vizuri wa ufundishaji.

Sita, Chuo Kikuu cha Al-Mustansiriyya – Iraq

Chuo hiki kilianzishwa mwaka 1227

Miladia mjini Baghdad, Iraq, na Khalifa Al-Mustansir wa Dola ya Abbasid. Kilitegemea mfumo mpana wa waqf uliogharamia huduma za matibabu, chakula cha bure, maktaba kubwa zenye vitabu adimu, pamoja na posho za nguo na fedha kwa wanafunzi na wahadhiri.

Al-Mustansiriyya kilikuwa chuo cha kwanza cha aina yake duniani kufundisha madhehebu yote manne ya sheria ya Kiislamu (Fiqh) chini ya paa moja, pamoja na sayansi za tiba, famasia, jiometri na hisabati.

Funzo kwa Tanzania katika kuen-deleza Waqf ya elimu

Vijana wengi wenye uwezo nchini Tanzania hawafiki chuo kikuu si kwa sababu ya upungufu wa akili, bali ni ukosefu wa fedha na mfumo mgumu. Udhamini huu unavunja mnyororo huo kwa kuruhusu vijana kusoma bila kuwaza fedha.

Kama inavyosisitizwa katika hotuba za usiku wa elimu, vijana hawa hawaendi kama watu binafsi bali wanakwenda kama ujumbe wa umma ili wakasome, wajifunze, na kurudi kujenga nchi yao badala ya kuchangia wimbi la kupoteza nguvu kazi (brain drain).

Swali la kwa nini Watanzania hawajiungi kuchangia kutoa udhamini (scholarship) wa kuwatoshe vijana pale Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM) kwa dola elfu tatu tu kwa miaka mitatu linagusa changamoto

kubwa zinazohusu jamii yetu.

Moja ya changamoto kuu ni uhaba wa uelewa wa mfumo wa Waqf. Wengi wamezoea mfumo wa mchango wa mara moja (haram-bee) badala ya kujenga mifumo ya kudumu (Endowment) ambayo mtaji wake unakaa na kuzaa faida ya kusomesha vizazi na vizazi bila mtaji wenyewe kuisha.

Changamoto nyingine ni utamaduni wa kutowekeza muda mrefu: Jamii nyingi huona misaada kuwa ni ile tu ya kulipia mahitaji ya haraka badala ya kuwekeza kwenye elimu ya juu kama mtaji wa kudumu wa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

Pia kuna ukosefu wa taasisi zinazoamini-ka: Ili watu watoe fedha zao, wanahitaji kuona mifumo iliyojipanga vizuri, yenye uwazi mkubwa, na yenye kusimamiwa kita-alamu kama inavyofanyika kupitia taasisi kubwa za nje - jambo ambalo linajengwa kwa nguvu hapa nchini kupitia jitihada za Awqaf Tanzania.

La mwisho ni hali ya vipaumbele: Wafanyabiashara na matajiri wakubwa mara nyingi hawajaelekezwa au kushawishika kisheria na kijamii kuelekeza sehemu ya utajiri wao kama wakfu wa kudumu wa elimu, jambo ambalo Mwenyekiti wa Awqaf Tanzania, Dkt. Kassim Hussein, anasema elimu juu ya waqfu ni kipaumbele katika mipango yao.

Mikakati ya kuiga ni pamoja na kuanzisha mifuko endelevu ya waqf wa kitaifa ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaofadhiliwa, kuhusisha sekta binafsi na hisani, kufanya uwekezaji wa kudumu wa rasilimali za ardhi, na kulenga wenye uhitaji halisi.





KATIKA ulimwengu wa uwekezaji, kila mtu anatamani kupata faida kubwa. Lakini je, tunafahamu kwamba matarajio ya faida kubwa yanaweza kuambatana na uwezekano mkubwa wa kupoteza fedha tulizowekeza?

Baadhi ya watu wamepoteza akiba zao kwa kuvutiwa na miradi inayoahidi faida kubwa ndani ya muda mfupi. Wengine wameepuka uwekezaji kabisa kwa kuhofia hasara, na hivyo kupoteza fursa za kukuza mali zao.

Katika elimu ya fedha, uhusiano kati ya hatari na faida huitwa risk and reward. Ni mojawapo ya kanuni muhimu ambazo kila anayetaka kuwekeza anapaswa kuzielewa.

Hatari (risk) ni uwezekano wa matokeo halisi ya uwekezaji kuwa tofauti na yaliyotarajiwa. Unaweza kupata faida ndogo, kuchelewa kulipwa au kupoteza sehemu au mtaji wote. Faida (reward) ni mapato yanayotarajiwa kutokana na uwekezaji, iwe kupitia gawio, ongezeko la thamani ya mali au mapato ya biashara.

Kwa kawaida, uwekezaji wenye uwezekano wa faida kubwa huhusisha kiwango kikubwa zaidi cha hatari.

Fikiria watu wawili wenye shilingi milioni 10 kila mmoja. Wa kwanza anawekeza katika mali yenye mabadiliko madogo ya thamani, wakati wa pili anawekeza katika kampuni changa inayotarajiwa kukua kwa kasi.

Wa pili anaweza kupata faida kubwa ikiwa kampuni itafanikiwa, lakini anaweza pia kupoteza mtaji wake ikiwa itashindwa.

Mambo ya kuzingatia

Kuna aina mbalimbali za hatari. Bei ya mali inaweza kushuka kutokana na mabadiliko ya soko. Mfumuko wa bei unaweza kupunguza uwezo wa fedha kununua bidhaa. Pia, unaweza kushindwa kuuza uwekezaji wako haraka unapohitaji fedha. Hii huitwa liquidity risk.

Jambo jingine muhimu ni muda. Fedha zinazohitajika kulipia ada ya mtoto mwaka ujao hazipaswi kuwekwa kwenye uwekezaji ambao

Zingatia haya kabla ya kufanya uwekezaji mkubwa

unaweza kuchukua miaka kadhaa kabla ya kufanikiwa kuuza.

Kwa uwekezaji wa muda mrefu, mtu anaweza kuwa na nafasi zaidi ya kuvumilia mabadiliko ya soko, ingawa muda mrefu hauondoi uwezekano wa hasara.

Je, unaweza kuvumilia hatari kiasi gani?

Vilevile, uwezo wa kuvumilia hatari hutofautiana. Kijana mwenye kipato cha uhakika na majukumu machache anaweza kuvumilia hasara ambayo ingemwathiri sana mzazi anayetegemewa na familia kubwa.

Kwa hiyo, kabla ya kuwekeza, jiulize: Fedha hizi nitazihitaji lini? Nikipoteza sehemu yake, maisha yangu yataathirika? Na ninaweza kuvumilia kushuka kwa thamani bila kufanya maamuzi ya papara?

Baada ya kuelewa mambo hayo, tunaweza kuangalia mikakati ya uwekezaji wenye hatari kubwa.

Ibrahim Khan, mwanzilishi mwenza wa Islamic Finance Guru, katika makala yake How To Do High Risk High Reward Investments Right, anashauri uwekezaji wa aina hiyo ufanywe kwa tahadhari na uwe sehemu ndogo ya mkusanyiko wa uwekezaji wa mtu.

Mikakati ya kupunguza hatari za uwekezaji

Mosi, tawanya mtaji wako

Kanuni hii huitwa diversification, yaani kutawanya uwekezaji katika mali, biashara au sekta mbalimbali.

Kwa mfano, badala ya kuweka mtaji wote katika kampuni moja changa, unaweza kuugawa katika uwekezaji tofauti kulingana na uwezo wako.

Lengo ni kupunguza athari za kushindwa kwa mradi mmoja, ingawa kutawanya uwekezaji hakuondoi hatari zote.

Pili, tenga sehemu ndogo kwa uwekezaji wa hatari kubwa

Islamic Finance Guru inapendekeza kiwango cha asilimia 10 hadi 30 ya mkusanyiko wa

uwekezaji kwa baadhi ya wawekezaji wenye uwezo na uzoefu.

Hata hivyo, huo si mwongozo unaofaa kila mtu. Mwenye akiba ndogo, madeni au majukumu makubwa anaweza kuhitaji kiwango kidogo zaidi au kuepuka uwekezaji huo.

Tatu, usiweke fedha katika biashara usiyoielewa.

Kabla ya kuwekeza, chunguza namna biashara inavyozalisha mapato, uzoefu wa waendeshaji wake, gharama, mikataba na uwezekano wa kushindwa.

Usivutiwe na ahadi za faida bila kuelewa fedha zako zitatumika kufanya nini.

Nne, chunguza watu unaowakabidhi fedha

Urafiki, undugu au maneno ya kuvutia si dhamana ya usalama wa uwekezaji.

Hakikishakampuni au msimamizi anaaminiwa, ana uzoefu, taarifa zinazoweza kuthibitishwa na leseni zinazohitajika kisheria.

Tano, zingatia uhalali wa uwekezaji kwa mujibu wa Sharia.

Kwa Muislamu, uwezekano wa kupata faida kubwa hauhalalishi kuwekeza katika shughuli zilizokatazwa.

Uwekezaji unapaswa kuepuka riba, kamari, udanganyifu na miamala yenye kiwango kisi-chokubalika chakutokuwa na uhakika (gharar).

Miongoni mwa fursa zinazoweza kuchunguzwa ni kuwekeza katika kampuni changa (startups), biashara ndogo na za kati, au miradi ya maendeleo ya majengo, kwa kutumia miundo inayokubalika kisheria.

Lakini kuitwa uwekezaji wa Kiislamu hakuamaanishi kwamba hauna hatari. Uhalali wa Sharia na usalama wa mtaji ni masuala mawili tofauti yanayohitaji kuchunguzwa.

Hatimaye, uwekezaji bora si ule unaoahidi faida kubwa zaidi, bali unaolingana na malengo yako, uwezo wako wa kifedha na hatari unazoweza kuzimudu.

Matumizi ya Akili Unde kwa mtazamo wa Kiislamu



Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulieleza kuwa nyuma ya kila mfumo wa Akili Unde (AI) kuna binadamu aliyeubuni, kuufundisha na kuamua namna utakavyotumika.

Kwa hiyo, wajibu wa kimaadili unabaki kwa binadamu, si mashine iliyoundwa. AI ni chombo kama zilizvyo zana nyingine, na uhalali wa matumizi yake hutegemea madhumuni na namna kinavyotumika. Sasa endelea na sehemu inayofuata...

Matumizi halali ya AI

Kwa ujumla, wanazuoni wa Kiislamu wa sasa wamekubaliana kuwa teknolojia ya Akili Unde (AI) inaruhusiwa katika Uislamu kwa kuwa ni chombo kilichoundwa na binadamu. Hata hivyo, hukumu yake ya kisharia hutegemea namna inavyotumika na madhumuni yake.

Matumizi ya AI yenye manufaa yanahimiza wa katika nyanja mbalimbali, zikiwamo elimu, utafiti, afya, tiba, uchumi na ustawi wa jamii.

Katika elimu ya Kiislamu, zana za AI hutumika kusaidia usomaji wa Qur'an, kuboresha usahihi wa usomaji wa Tajwidi, kujifunza lugha ya Kiarabu na taaluma mbalimbali za Kiislamu. Aidha, teknolojia hiyo hutumika katika uchunguzi wa kimatibabu na utoaji wa huduma za afya.

Teknolojia ya AI pia inaweza kutumika katika utafiti na ugunduzi wa kisayansi, utengenezaji wa vifaa vya kuwasaidia watu wenye ulemavu, uhakiki wa vyakula na bidhaa ili kuhakikisha uhalali wake, pamoja na kurahisisha uendeshaji wa biashara halali kwa njia za kiotomatiki.

Matumizi mengine halali ya AI ni kukokotoa na kusambaza zaka, kutafsiri maandiko ya Kiislamu katika lugha nyingine, na kubaini udang-

anyifu katika mifumo ya benki za Kiislamu.

Matumizi haramu ya AI

Licha ya manufaa mengi ya Akili Unde, teknolojia hiyo inaweza kutumiwa kwa njia zinazokiuka maadili na misingi ya sheria ya Kiislamu. Miongoni mwa matumizi hayo ni kutengeneza au kuhariri picha, video na sauti ili kumwonesha mtu akisema au akifanya jambo ambalo hakulisema wala kulifanya, kwa lengo la kupotosha umma au kuharibu sifa yake.

Matumizi mengine ni kunakili sauti au sura ya mtu bila idhini yake, kutengeneza maudhui ya ponografia au yanayokiuka maadili, na kutumia mifumo ya AI katika kamari na ubashiri. Vilevile, matumizi yasiyofaa ya AI ni pamoja na kuunda wanazuoni bandia mitandaoni, kutengeneza fat-wa za uongo au kusambaza maudhui ya kidini yanayopotosha.



Ni huzuni ndoa inapogeuka pango la kifo

Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya watu wakiwajeruhi au kuwaua wenza wao, ambao waliwahi kuwaahidi kuwapenda, kuwalinda na kuishi nao katika shida na raha.

Hali hii inazua mjadala mpana kuhusu thamani ya uhai, usalama ndani ya familia na namna migogoro ya ndoa inavyopaswa kushughulikiwa. Inasikitisha kuona ndoa, ambayo inapaswa kuwa kimbilio la faraja na usalama, inageuka kuwa chanzo cha hofu, majeraha na hata vifo.

Tofauti za kimawazo, ugomvi, hasira, kutoelewana au wivu haviwezi kuhalalisha kumduru au kumuua mtu mwingine. Kwa msingi huo, ukatili ndani ya ndoa haupaswi kuvumiliwa, kuhalalishwa wala kufichwa kwa kisingizio cha kulinda ndoa.

Tatizo huanza pale mmoja wa wanandoa anapoamini kuwa ana haki ya kumtisha, kumdhibiti au kumwadhibu mwenzake anapokosea au anaposhindwa kutimiza matarajio yake. Mtazamo huo ni hatari kwa sababu unageuza ndoa kutoka katika ushirikiano wa watu wawili na kuifanya kuwa uhusiano wa vitisho.

Ni muhimu kufahamu kuwa hasira ni hisia za kibinadamu ambazo kila mtu anaweza kukumbana nazo katika maisha ya kila siku. Hata hivyo, hasira zisizodhibitiwa zinaweza kusababisha ndoa kuvunjika au kupelekea wanandoa kufanya maamuzi yenye madhara.

Mtu anapokumbwa na hasira, anapaswa kujiondoa kwa muda katika mazingira ya mabishano, kutafuta ushauri au kutumia njia za amani kutatua tatizo.

Jamii isinyamazie dalili za ukatili

Jambo jingine linalopaswa kuangaliwa kwa kina ni namna jamii inavyoshughulikia taarifa za ukatili ndani ya familia. Wakati mwingine, vitendo vya unyanyasaji, vitisho na vipigo hufumbiwa macho au kufichwa kwa kisingizio kwamba matatizo ya ndoa ni siri za wanandoa.

Mtazamo huu unaweza kuwanyima

waathiriwa fursa ya kupata msaada kwa wakati na hivyo kuruhusu vitendo vya ukatili kuendelea. Ni muhimu kutofautisha kati ya kulinda faragha ya familia na kuficha vitendo vinavyohatarisha maisha.

Familia, majirani, viongozi wa dini na jamii husika wana wajibu wa kuchukulia taarifa za ukatili kwa uzito na kuwasaidia waathiriwa kupata ulinzi unaohitajika. Pale ambapo kuna vitisho au hatari ya madhara ya kimwili, usalama wa mtu unapaswa kupelelewa kipaumbele.

Vilevile, waathiriwa hawapaswi kulaumiwa kwa ukatili wanaofanyiwa, wala kulazimishwa kubaki katika mazingira hatari kwa kisingizio cha kulinda ndoa. Kuomba msaada si udhaifu, na kutafuta usalama si kuvunja maadili ya dini au ya jamii, bali ni hatua muhimu ya kulinda uhai na utu.

Ndiyo maana Mwenyezi Mungu ameruhusu talaka pale ambapo wanandoa wameshindwa kuendelea kuishi pamoja kwa amani. Mwenyezi Mungu anasema: “Talaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri.” Aidha, Mwenyezi Mungu anaendelea kusema: “Na ikiwa mna hofia kuwa hawataweza kusimamisha mipaka ya Allah, basi hakuna lawama juu yao kwa kile ambacho mke atajikomboa nacho

(khul’u)...” [Qur’an, 2:229].

Pamoja na mambo mengine, aya hiyo inaruhusu pia khul’u, yaani mke kuomba ndoa ivunjwe kwa kufuata utaratibu unaotambuliwa na sharia. Hivyo, aya hiyo inaunga mkono hoja kwamba ndoa inaposhindikana kuendelea, ni bora wanandoa kuachana kwa heshima kuliko kuendeleza uhusiano unaoweza kusababisha madhara.

Tahadhari ya ukatili na hatua za kuchukua

Katika kushughulikia migogoro ya ndoa, ni muhimu kutambua kuwa migogoro ni sehemu ya kawaida ya maisha na haiwezi kuepukika, hata kwa wanandoa wanaopen-dana na wanaotaka kudumisha upendo wao.

Hatua ya kwanza katika kushughulikia migogoro ni kuwalea vijana katika mazingira yanayowafundisha kuheshimu wengine, kuwa wavumilivu na kutatua tofauti zao kwa njia za amani badala ya kutumia nguvu.

Vijana wanapojifunza mapema kuwa tofauti za mawazo hazipaswi kutatuliwa kwa vipigo au vitisho, hujenga msingi imara wa kuanzisha na kudumisha uhusiano mwema wanapokuwa watu wazima.

Aidha, elimu ya ndoa inapaswa kuwajengea wanandoa uelewa kuhusu umuhimu wa mawasiliano bora, kusikilizana na kutafuta suluhu zinazozingatia haki za kila mmoja. Pale migogoro ya ndoa inapokuwa mikubwa, ushauri wa kitaalamu unaweza kusaidia kupata suluhu, mradi tu mazingira yawe salama.

Hata hivyo, kunapokuwa na ukatili au vitisho vya moja kwa moja, hatua za kujilinda zinapaswa kupewa kipaumbele badala ya kumlazimisha mwathiriwa kuendelea kuishi katika mazingira hatarishi.

Vilevile, viongozi wa dini wana wajibu wa kutoa mafundisho yanayosisitiza umuhimu wa kulinda uhai na utu wa binadamu. Kupitia mahubiri na mafundisho yao, wanapaswa kuisitiza kuwa upendo wa kweli haujengwi kwa vipigo, vitisho wala unyanyasaji, bali kwa kuheshimiana, kuwajibika na kujali usalama wa kila mmoja.



ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Kubeba Janaza na kulisindikiza hadi kaburini: Sunnah, adabu na mafunzo

SEHEMU YA

10

Baada ya Muislamu kuoshwa, kuvikwa sanda na kuswaliwa, hatua inayofuata ni kumpeleka kwenye makazi yake ya barzakh: kaburini. Hii ni hatua yenye ujumbe mkubwa sana kwa walio hai. Mtu anayebeba leo alikuwa jana akiishi pamoja nasi, akipanga maisha yake, akicheka na kuzungumza. Lakini leo anabebwa juu ya mabega ya watu wengine akielekea mahali ambapo kila mwanadamu ataelekea. Kwa kuona hilo, Uislamu umetufundisha namna ya kushiriki katika safari hii kwa heshima, utulivu na kumkumbuka Allah.

Fadhila ya kubeba na kusindikiza janaza

Kumsindikiza Muislamu mwenzako katika Janaza ni miongoni mwa haki zake.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Mwenye kushuhudia Janaza mpaka ikaswaliwa, atapata Qirat moja. Na mwenye kulishuhudia mpaka ikazikwa, atapata Qirat mbili.” [Bukhari na Muslim].

Hii inaonesha kuwa thawabu ya kushiriki Janaza haimaliziki kwenye Swala pekee, bali inaendelea mpaka mazishi yanapokamilika.

Kubeba Janaza ni Sunnah

Katika zama za Swahaba, walikuwa wakishiriki kubeba jeneza kwa mikono yao. Hili ni jambo linaloonesha unyenyekevu;

mshikamano; kumuenzi marehemu; na kumkumbuka mwisho wa maisha.

Leo magari yamerahisisha usafiri, na kutumia gari kwa sababu ya umbali au mazingira ni jambo linaloruhusiwa. Lakini hilo lisitufanye kupoteza roho ya kushiriki na kuhudhuria.

Adabu wakati wa kubeba Janaza:

Kwanza, anayeshiriki katika msafara wa Janaza anatakiwa awe na utulivu. Msafara wa mazishi si mahali pa mazungumzo ya dunia, vicheko au simu zisizo za lazima. Ni wakati wa kutafakari na kumuomba marehemu.

Pili, inatakiwa kuepuka maombolezo yasiyo ya kisharia. Uislamu umetufundisha subira katika msiba. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Si katika sisi mwenye kupiga mashavu, kurarua nguo na kuita kwa mwito wa kijahili.” [Bukhari na Muslim].

Kulazimika kwa huzuni ni jambo la kibinadamu, lakini Uislamu unakataza vitendo vinaavyoonesha kutoridhika na qadar ya Allah.

Tatu, kumtaja Allah na kumwomba Marehemu. Katika baadhi ya maeneo, watu wamezo-ea kutamka dhikri maalumu kwa sauti moja wakati wa kubeba janaza. Wanazuoni wameto-fautiana kuhusu baadhi ya aina hizo za dhikri za pamoja.

Jambo la msingi ni kwamba mwenye kusindikiza janaza anapaswa kuwa katika hali ya kumkumbuka Allah na kumuomba marehemu, bila kugeuza mazishi kuwa tukio la mayowe au sauti na desturi zisizo na msingi.

Je, ni sunnah kutembea mbele au nyuma ya Janaza?

Wanazuoni wamezungumzia nafasi ya anayefuatana na janaza. Imepokewa katika baadhi ya hadith kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) na Swahaba walitembea

nyuma ya janaza, na katika riwaya nyingine imetajwa mbele yake.

Kwa hiyo, suala hili lina nafasi ya ikhtilafu ya wanazuoni. Jambo muhimu zaidi si nafasi ya mtu katika msafara, bali ni kuhudhuria kwa unyenyekevu na kutekeleza haki ya marehemu.

Kasi ya kupeleka Janaza

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Harakisheni janaza.” [Bukhari na Muslim]. Maana yake ni kutochelewesha mazishi bila sababu.

Lakini kuharakisha hakumaanishi kukosa utaratibu au kukimbia kiasi cha kuondoa heshima ya mazishi. Unaotakiwa ni mwendo wa kawaida wenye lengo la kumfikisha marehemu kwenye maziko kwa wakati unaofaa.

Makosa yanayoonekana katika jamii

Baadhi ya mambo yanayojitokeza, miongoni mwa makosa, ni watu wengi kuja kwa ajili ya mazungumzo kuliko kumuomba marehemu, kupiga picha na kurekodi video za msafara wa mazishi na kuonesha huzuni kwa mayowe na vilio vya kupita kiasi.

Makosa mengine ni kufanya mazishi kuwa sehemu ya kujionesha kijamii, kuhudhuria kwa lengo la kuondoa lawama; naye alikuwepo; kuchelewesha mazishi kwa sababu zisizo za msingi na watu kuondoka mara baada ya Swala ya Janaza bila sababu, wakikosa fadhila ya kushiriki mpaka mazishi.

Funzo kubwa kutoka katika Janaza

Msafara wa mazishi ni mawaidha yanayotembea. Allah Mtukufu amesema: “Kila nafsi itaonja mauti.” [Qur'an, 3:185]. Mtu anayelala ndani ya jeneza leo alikuwa na mipango kama sisi. Alikuwa na matumaini, hofu na mambo aliyokuwa akiyafikiria.

Lakini yote yaliachwa nyuma. Kilichobaki ni yale aliyoyatanguliza mbele yake.

Hitimisho

Kuhudhuria maziko na kusindikiza Janaza si tu kumuenzi marehemu, bali ni kumkumbusha aliye hai kuhusu mwisho wake.

Mwenye kusindikiza Janaza kwa unyenyekevu hufaidika kwa mambo mawili: humsaidia ndugu yake kwa dua na uwepo wake na hujikumbusha kwamba yeye pia siku moja atakuwa katika safari hiyo.

Hivyo, tuyafanye maziko na kuhudhuria Janaza kuwa ibada ya heshima, utulivu na kumkumbuka Allah.

SEHEMU YA

1

Miaka mitatu imepita, lakini damu na machozi bado havijakauka. Mauaji ya kimbari yanaendelea huku Gaza ikien-delea kushambuliwa kwa mabomu yasiyokoma. Mauaji ya Waislamu katika ardhi hiyo tukufu yanaonekana kutokuwa na mwisho, pengine hadi watu wote wa Gaza watakapomalizwa! Hakuna siku inayopita bila mashambulizi ya anga, kupoteza wapendwa, kuporomoka kwa majengo, au kuharibiwa kabisa kwa kambi za wakimbizi. Hakuna mapatano ya kunusuru maisha ya raia, hakuna usitishaji wa mapigano wala uingiliaji kati wenye tija.

Ndugu zangu katika imani, sasa imetimia miaka mitatu tangu kuanza kwa mauaji ya kimbari yanayoendelea Gaza, lakini swali linabaki kuwa lilelile: Suluhisho la janga hili ni lipi?

Gaza ni kioo

Mauaji ya kimbari yanayoendelea Gaza ni kioo kinachoakisi hadhi, heshima na kujitolea kwa umma wa Waislamu. Vilevile, yanaweka wazi majeraha makubwa ambayo Waislamu duniani kote wameyapata tangu walipopoteza dola yao ya Kiislamu.

Aidha, mauaji hayo yanafichua unafiki, ubalakala na uadui mkubwa dhidi ya Uislamu unaodhihirishwa na mataifa ya Magharibi. Hali hiyo pia inafichua uhalisia wa sheria za kimataifa na taasisi zake, ambazo zimeonekana kuwa dhaifu, zisizo na uzito na zinazofuata ajenda za mataifa hayo ya kikoloni.

Kinachoumiza zaidi ni kushindwa kwa mataifa ya Waislamu duniani kuilinda Palestina na watu wake, licha ya kumiliki majeshi na silaha nzito. Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba baadhi ya mataifa hayo yana ushirikiano mzuri na mabeberu wa Magharibi!

Miaka mitatu ya mateso Gaza, nini kifanyike?



Kushindwa kuchukua hatua madhubuti za kuwalinda ndugu zao Wapalestina hatimaye kumeyafanya mataifa hayo kujikuta yakilinda bila kukusudia dola haramu ya Kizayuni, ambayo inaendeleza kampeni ya maangamizi na kusababisha njaa miongoni mwa wakazi wa Gaza. Hata hivyo, katikati ya mazingira hayo magumu, watu wa Gaza wameendelea kusimama imara na kukataa kusalimu amri. Kadhalika, umma wa Waislamu duniani kote haujakaa kimya katika kuwaunga mkono.

Badala yake, unafuata kwa vitendo mafundisho ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) aliyesema: “Mfano wa waumini katika kupendana, kuhurumiana na kujali hisia za wenzao ni kama mwili mmoja; kiungo chochote kinapouma, mwili mzima huumia kutokana na kukosa usingizi na homa.” [Sahih Bukhari].

Kile kinachoitwa “vita” kimegeuka kuwa mauaji ya kimbari dhidi ya Waislamu wa Gaza, ambao wanaonekana kulengwa kwa sababu ya imani yao. Hali hii inatukumbusha kisa cha Watu wa Ukhdud (Mahandaki), ambao Allah amewataja katika sura nzima ya Qur’an.

Allah anasema: “Na hawakuwachukia isipokuwa kwa vile wamemwamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa.” [Qur’an,

85:8]. Chuki hii inachochewa zaidi na husuda na hofu. Ni chuki inayowafanya baadhi ya watu kuutambua ukweli, lakini wakaukataa na hatimaye kuwachukia wale wanaoutetea.

Vilevile, chuki hii huchochewa na hofu iliyo ndani ya nafsi za wenye husuda kwamba huenda ukweli ukadhihirika na kufichua upotofu wao.

Allah Ta’ala amebainisha hilo aliposema: “Wengi miongoni mwa Watu wa Kitabu wanatamani lau wangelikurudisheni nyinyi waumini kwenye ukafiri kwa sababu ya husuda iliyomo katika nafsi zao, baada ya ukweli kubainika wazi kwao...” [Qur’an, 2:109].

Muumini daima hutambulika kwa unyenyekevu wake kwa Muumba katika mambo yote. Muislamu huweka kando matamania ya nafsi yake na hamuabudu yeyote isipokuwa Allah ‘Azza wa Jallah’.

Kwa hiyo, licha ya uharibifu mkubwa uliotokea Gaza, ishara za amri na rehema za Mwenyezi Mungu zinaendelea kudhihirika. Watu wa Gaza wanaendelea kusimama imara kwa subira, watoto wanaendelea kuzaliwa, na familia zinaendelea kushikilia matumaini.

Watu wa Gaza, ambao wamepoteza takriban kila kitu, bado wanaendelea kutangaza kwa maneno na vitendo kwamba kamwe hawataia-cha imani yao.

Vijana hatuhitaji hamasa pekee bali 'mentorship'

FIKIRIA kijana aliyemaliza chuo kikuu na kupata shahada yake. Anaalikwa kwenye kongamano kuhusu fursa za kujiiajiri. Wazungumzaji wanatoa hotuba kali kuhusu biashara, uwekezaji na namna vijana wanavyoweza kujikwamua kiuchumi. Anatoka ukumbini akiwa na hamasa kubwa. Anaona fursa ziko kila mahali na anajisemea, kumbe fedha zipo! Lakini anapofika nyumbani, anakutana na swali moja gumu: Nianzie wapi? Hajui namna ya kuchagua biashara, kuchunguza soko, kupata mtaji au kuwafikia wateja. Hatimaye, hamasa inapungua na maisha yanaendelea kama kawaida.

Hali hiyo inaweza pia kumkuta kijana anayesikia kuhusu fursa nyingi za kazi za mtandaoni, lakini anapoanza kuzitafuta anakutana na taratibu, mahitaji ya ujuzi na changamoto asizojua namna ya kuzitatua.

Au mtu aliyesilimu na kupokewa kwa fura ha msikitini, lakini baadaye akaachwa peke yake bila mtu wa kumfundisha kuswali, kujifunza Qur'an na kuishi maisha yake mapya ya Kiislam.

Mifano hii inanifanya niamini kwamba sisi vijana hatukosi hamasa na taarifa za fursa pekee; mara nyingi tunakosa watu wa kutuongoza hatua kwa hatua ili kuzitumia fursa hizo.

Ndiyo maana ninadhani tunahitaji kuimarisha utamaduni wa mentorship, yaani malezi elekezi yanayomunganisha mtu mwenye uzoefu na mwingine anayehitaji maarifa, ushauri na mwongozo katika kufikia

malengo yake.

Tofauti kati ya mhamasishaji na mlezi elekezi ni kubwa. Mhamasishaji anaweza kukufanya uamini kwamba unaweza kufanikiwa. Mlezi elekezi anakusaidia kuelewa namna ya kufanya hivyo.

Faida za mentorship

Malezi elekezi au mentorship, kiufupi, ni uhusiano wa kujifunza unaomwezesha mtu mwenye uzoefu kumsaidia mwingine kupitia mawasiliano, ushauri na mwongozo wa karibu.

Kwa mtazamo wangu, faida yake ya kwanza ni kutusaidia kugeuza maarifa kuwa vitendo.

Tunaweza kusoma vitabu vingi kuhusu biashara, lakini bado tukashindwa kujua namna ya kupata mteja wa kwanza. Tunaweza kusoma kuhusu uandishi wa habari, lakini tukahitaji mwandishi mwenye uzoefu atuonyeshe namna ya kutafuta habari na kuwasiliana na vyanzo.

Mlezi elekezi anatusaidia kuunganisha kile tunachokijua na namna ya kukitumia katika mazingira halisi.

Faida ya pili ni kutuepusha na makosa ambayo wengine tayari wameyafanya. Si lazima kila mmoja wetu ajifunze kwa kupoteza fedha, muda au fursa. Tunaweza kujifunza kutokana na makosa na uzoefu wa waliotutangulia.

Tatu, ushauri elekezi unatusaidia kuona udhaifu ambao sisi wenyewe hatuuoni.

Mara nyingi tunapokuwa na wazo tunalolipenda, tunaweza kushindwa kuona mapungufu yake. Mtu mwenye uzoefu anaweza kutuuliza maswali magumu, kutuonyesha hatari na kutusaidia kufikiria kwa upana zaidi.

Mlezi mzuri si yule anayesifu kila wazo letu, bali anayethubutu kutueleza ukweli kwa nia ya kutuendeleza.

Nne, ushauri elekezi unajenga kujiamini na kutusaidia kuvumilia changamoto.

Katika simulizi yake aliyoiita My Two Mentors, mwandishi mmoja wa mtandaoni, Amjad Shaykh anaeleza namna binamu zake wawili walivyomsaidia alipokuwa kijana mwenye maswali na changamoto kuhusu

imani yake.

Hawakumpa majibu pekee. Walimsikiliza, walimvumilia na kumpa nafasi ya kujifunza kwa utaratibu.

Hapa tunajifunza kwamba mlezi elekezi si mtu wa kutoa maagizo tu. Ni mtu wa kusikiliza, kututia moyo na kutusaidia kufanya maamuzi kwa uelewa.

Tano, mentorship inaweza kutufungulia milango ya fursa.

Mtu mwenye uzoefu anaweza kutuunganisha na wataalamu, kutuelekeza kwenye mafunzo au kutusaidia kutambua nafasi ambazo tusingezijua wenyewe.

Hata hivyo, si lazima mlezi wetu awe tajiri, maarufu au mwenye cheo kikubwa. Tunaweza kujifunza hata kwa mtu aliyetutangulia hatua chache tu. Pia, si lazima tutegemee mlezi mmoja kwa kila jambo. Tunaweza kujifunza biashara kwa mfanyabiashara, taaluma kwa mtaalamu na dini kwa mwana-zuoni mwenye maarifa.

Lakini kuna faida nyingine ambayo ningependa kuisisitiza: ulezi elekezi unajenga uwajibikaji.

Ni rahisi kupanga malengo na kuyaacha. Lakini unapokuwa na mtu anayekuuliza umefikia wapi, changamoto gani umekutana nazo na hatua gani unafuata, unapata msukumo wa kutekeleza mipango yako.

Ndiyo maana ningependa kuona taasisi zetu za Kiislamu, misikiti na jumuiya za vijana zikiandaa programu za malezi elekezi. Tuna wafanyabiashara, wanazuoni na wataalamu wengi ambao uzoefu wao unaweza kuwasaidia vijana.

Mentorship iheshimu mipaka ya sharia

Bila shaka, programu hizo zinapaswa kuheshimu mipaka ya Sharia. Wasichana wapate walezi elekezi wanawake inapowezekana, na pale ambapo wanaume wanatoa mwongozo kwa wasichana, ufanyike katika mazingira ya wazi, kwa makundi na bila faragha isiyofaa. Sisi vijana pia tunapaswa kuelewa kwamba malezi elekezi hatufanyii kazi. Anatuelekeza, lakini jukumu la kuchukua hatua linabaki kwetu.

Nimalizie kwa kutoa wito kwa viongozi wetu: Msituambie tu kwamba fursa zipo. Tusaidieni pia kujua namna ya kuzifikia.

Maana wakati mwingine kinachomtenganisha kijana na mafanikio si ukosefu wa uwezo au juhudi, bali ni kukosa mtu mwenye uzoefu wa kumwonyesha njia.

Chukua tahadhari hizi unapomnunulia mtoto baiskeli

KUENDESHA baiskeli ni miongoni mwa michezo inayopendwa sana na watoto. Kwa baadhi yao, kupata baiskeli ni zawadi kubwa inayowapa furaha, uhuru wa kutembea na nafasi ya kucheza pamoja na wenzao.

Mbali na burudani, kuendesha baiskeli kuna manufaa kwa afya. Kunasaidia kuimarisha misuli, kujenga uwezo wa kuweka mwili katika usawa, kuongeza uratibu wa viungo na kumzoesha mtoto kufanya mazoezi.

Hata hivyo, furaha hiyo inaweza kugeuka huzuni endapo mtoto ataanguka, kugongwa na gari au kupata majeraha wakati wa kuendesha baiskeli.

Kwa hiyo, mzazi hapaswi kuishia kumnunulia mtoto baiskeli na kumwachia aendeshe popote anapotaka. Anapaswa pia kumfundisha kanuni za usalama na kuhakikisha mazingira anayochesha hayamweki katika hatari zisizo za lazima.

Zifuatazo ni hatua muhimu za kumlinda mtoto anapoendesha baiskeli.

Mosi, mhakikishie kofia maalumu ya kujikinga kichwani

Kofia ya usalama, inayojulikana kama helmet, ni miongoni mwa vifaa muhimu zaidi kwa mwendesha baiskeli.

Matumizi sahihi ya kofia hiyo hupunguza hatari ya majeraha makubwa ya kichwa na ubongo wakati wa ajali. Kofia iwe na ukubwa unaomfaa na inayokaa vizuri bila kuyumba. Kofia inapaswa kufunika sehemu ya juu ya paji la uso, huku mkanda wake ukiwa umefungwa vizuri chini ya kidevu.

Pili, mnunulie baiskeli inayolingana na umri na ukubwa wake

Baadhi ya wazazi hununua baiskeli kubwa kwa matarajio kwamba mtoto ataendelea kuitumia hata atakapokua.

Hata hivyo, baiskeli kubwa kupita kiasi inaweza kumfanya mtoto ashindwe kuidhibiti, kufikia breki au kusimama kwa usalama.

Ni vema kuwashirikisha watoto wakati wa kuchagua baiskeli ili kuhakikisha wanaweza kuifikia usukani, kutumia breki na kuweka miguu chini ipasavyo.

Tatu, kagua baiskeli kabla ya mtoto kuanza kuiendesha.

Baiskeli yenye breki mbovu, tairi lisilo na upepo wa kutosha au usukani uliolegea inaweza kusababisha ajali hata kama mtoto ana uzoefu wa kuiendesha.

Mzazi anapaswa kukagua breki, magurudu-

mu, mnyororo na sehemu nyingine muhimu mara kwa mara. Mtoto naye afundishwe kutambua dalili za hitilafu na kutoa taarifa kabla hajaendelea kuitumia.

Nne, mchagulie mavazi na viatu vina-vyofaa

Nguo zinazong'aa au zenye rangi zinazoonekanakwaurahisizina-weza kusaia watumiaji wengine wa barabara kumwona mtoto.

Epuka mavazi marefu au mapana yanayoweza kunaswa na mnyororo au magurudumu.

Mtoto avae viatu vinavyofunika vidole na kushika miguu vizuri, badala ya kandambili zinazoweza kuteleza au kutoka wakati wa kuendesha.

Tano, mchagulie sehemu salama ya kuendesha

Si kila eneo linafaa kwa mtoto kuendesha baiskeli. Barabara zenye magari mengi, malori,

bodaboda au makutano hatarishi zinapaswa kuepukwa, hasa kwa watoto wadogo.

Ni vizuri kuanza katika maeneo yenye nafasi ya kutosha, yasiyo na msongamano wa magari na yaliyo mbali na hatari kama mitaro iliyo wazi.

Sita, mfundishe kanuni za barabarani

Mtoto anapaswa kujua umuhimu wa kuangalia magari kabla ya kuvuka, kutambua alama za barabarani na kuwaheshimu watumiaji wengine wa njia.

Mfundishe kutumia breki kwa usahihi, kupunguza mwendo anapokaribia makutano na kutokuendesha huku akitumia simu au kufanya vitendo vina-vyomwondolea umakini.

Watoto wadogo wasiruhusiwe kuendesha kwenye barabara zenye magari bila usimamizi unaofaa.



Hakika, madhambi humnyima mtu riziki

Katika sura ya Saba' (Qur'an, 34:15–17), Allah anaeleza jinsi alivyowabariki watu wa Saba' (Yemen) kwa kuwapa ardhi yenye rutuba na neema nyingi, zikiwamo bustani mbili kubwa na nzuri.

Allah aliwaambia: "...kuleni katika riziki ya Mola wenu na mshukuruni. Ni mji mzuri na Mola ambaye ni Mwingi wa kusamehe. Lakini waka- kengeuka, basi tukawapele- kea mafuriko ya mabwawa, na tukazibadilisha bustani zao mbili kwa bustani mbili zenye matunda mac- hungu, miti ya mivinje na kiasi kidogo cha mikunazi. Hayo tuliwalipa kwa vile walivyokufuru. Na hatuad- hibu isipokuwa asiye na shukrani?"

Mafundisho ya aya

Aya hizi zinaeleza wazi jinsi neema zina- vyoweza kugeuka kuwa adhabu kutokana na maasi. Pia, zinaashiria kuondoka kwa neema

ambazo watu walikuwa wakizifurahia na mai- sha yao kugeuka kuwa ya maumivu na misiba.

Allah ametaja kanuni aliyowawekea wan- adamu aliposema: "Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi hali ya watu mpaka wao wabadil- ishe yaliyomo katika nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu akiwakusudia watu adhabu hakuna wa kuirudisha..." [Qur'an, 13:11].

Pia, mshairi mmoja alisema: "Ukiwa kwe- nye neema, basi ilinde na uitunze. Hakika dhambi huondoa neema. Na izungushie ulinzi kwa kumtii Mola wa waja, kwani Mola wa waja ni Mwepesi wa kuleta adhabu."

Miongoni mwa neema zinazoweza kuon- dolewa kutokana na kukithiri kwa madhambi ni usalama na riziki. Qur'an inasema: "Na Allah amepiga mfano wa mji (wa Makka) uliokuwa salama na wenye utulivu, ukiwa unapata riziki yake kwa wingi kutoka kila mahali, kisha ukazikufuru neema za Allah, basi Allah akauonjesha vazi la njaa na hofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafan- ya." [Qur'an, 16:112].

Na katika hadith iliyonukuliwa na Imam Ahmad, Mtume (rehemana amani zimshukie) amesema: "Hakika mtu hunyimwa riziki kwa sababu ya dhambi aliyoifanya."

Kushindwa mbele ya maadui

Hakuna shaka kwamba madhambi na maasi yana madhara makubwa yanayoweza kuvuruga na kuharibu jamii kiuchumi, kim- wili na kiroho. Madhara yake hayaishii kwa mtu aliyefanya dhambi pekee, bali yanaweza kuenea na kuwaathiri watu wengine pia.

Miongoni mwa madhara hayo ni kushind- wa vibaya mbele ya maadui katika mapam- bano, na kukumbwa na udhaifu na unyonge. Tafakari, ni nini kilichosababisha Maswaha- ba (Allah awaridhie wote), ambao tayari wali- kuwa wamepata ushindi katika vita vya Uhud kushindwa ghafla?

Allah anasema: "Na kwa hakika Mwenyezi Mungu alitimiza ahadi yake kwenu mlipoku- wa mkiwaua maadui kwa idhini yake, mpaka mliposhindwa na kuzozana katika amri (ali- yokupeni Mtume) na mkaasi baada ya Yeye

kukuonyesheni yale mliyoyapenda (mali). Miongoni mwenu walikuwepo waliotaka dunia, na miongoni mwenu walikuwepo wali- otaka Akhera. Kisha akawaepusha nao (hao maadui) ili akujaribuni..." [Qur'an, 3:152].

Allah aliwapa ushindi kama alivyoahidi, lakini walipoasi amri ya Mtume waligeuka kutoka washindi na kuwa walioshindwa. Hawa walikuwa watu wema waliotenda mambo mengi makubwa na matukufu, laki- ni walipokosea, Allah aliwanyima ushindi ili watu wajifunze kutokana na yaliyowapata.

Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar (Allah amridhie yeye na baba yake) kwamba alim- sikia Mtume wa Allah akisema: "Mtakapo- fanya biashara ya 'Inah' (aina ya biashara yenye riba) na mkashika mikia ya ng'ombe (ufugaji), mkajishughulisha na kilimo pekee na mkaacha Jihad, Allah atawatawalishia unyonge (atawafanya muwe dhalili) mpaka mrudi katika dini yenu." [Ahmad na Abu Daudi].

Katika hadith nyingine Mtume amese- ma: "Mataifa mengine yanakaribia kuitana ili yawashambulie (na kupora ardhi yenu) kama walaji wanavyoitana kwenye sinia lao la chakula."

Mtu mmoja akauliza: "Je, wakati huo tut- akuwa wachache?" Mtume akajibu: "Hapana, mtakuwa wengi wakati huo, lakini mtakuwa kama povu la mafuriko. Na hakika Allah ata- ondoa hofu katika vifua vya maadui zenu, na ataingiza udhaifu katika mioyo yenu."

Wakauliza: "Ewe Mjumbe wa Allah! Ni udhaifu gani huo?" Mtume akasema: "Ni kupenda dunia na kuchukua kifo." [Abu Dau- di].

Kupoteza afya na uzima

Miongoni mwa neema ambazo zinaweza kupotea kutokana na madhambi na maasi ni afya na uzima. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hauenei uchafu (wa zinaa) kwa watu kisha wakautangaza waziwa- zi isipokua yataenea kwao magonjwa ya tauni na magonjwa mengine ambayo hayakuwepo kwa wazee wao waliopita." [Ibn Majah].

Uharibifu wa mazingira na ukame

Maovu husababisha uharibifu katika nchi na kuzuia mvua kunyesha. Allah anasema: "Ufisadi umedhihiri nchi kavu na baharini kwa sababu ya yale yaliyochumwa na miko- no ya watu, ili (Allah) awaonjeshe baadhi ya waliyoyatenda, huenda wakarejea." [Qur'an, 30:41].

Kamati zinapokuwa kikwazo kwa taasisi za wanachama

NIMEBAHATIKA kuwa mwanachama wa taasisi kadhaa za hiari, hususan za kidini, na kwa uzoefu wangu ni nadra kuona kamati ndogo za vitengo katika taasisi hizi ziki-fanya kazi kwa ufanisi unaotarajiwa. Taasisi moja ninayoifahamu ina uongozi wa taifa, kanda, vituo hadi misikiti. Kila ngazi, baada mwenyekiti, katibu na mweka hazina, kuna kamati za elimu, afya, mipango, uchumi na kadhalika. Ufanisi, kama upo, ni asilimia 5 pengine. Kamati hizo ni kama zimekufa. Zipo kwenye katiba, zinatajwa katika vikao na zina viongozi walioteuliwa au kuchaguliwa, lakini hakuna kinachofanyika. Taasisi nyingine ina kliniki. Hata huko, kama kuna ufanisi ni kwa juhudi za mtu sio kamati hizo zilizobatizwa kliniki. Kamati zinaposhindwa kufanya kazi, tuna-laumiana "Hamtaki kujitolea kwenye dini." "Hamrudishi kwa umma." "Hamna shukrani kwa neema mlizopewa na Mwenyezi Mungu." Lakini hebu tujiulize kwa makini: Je, tatizo ni watu tunaowateua wajumbe wa kamati hizi, au mfumo wenyewe tunaoutumia kundesha taasisi?

Mfumo wa kamati

Tatizo kubwa ninaloliona katika mfumo wa kamati ni namna unavyogawa uwajibikaji kwa watu wengi kiasi kwamba wakati mwingine haku-na anayejisikia kuwajibika moja kwa moja.

Kamati inapokuwa na wajumbe saba, tisa au zaidi, kila mmoja anajua kwamba jukumu fulani si lake peke yake. Asipolifanya, anaweza kudhani wengine watalifanya. Na wengine nao wanaweza kuwa na fikra hizohizo. Mwishowe, kazi inabaki bila kufanyika, huku kila mmoja akiwa na sababu ya kueleza kwa nini hakufanya.

Katika saikolojia ya kijamii, hali hii inahusishwa na dhana ya diffusion of responsibility, yaani mtawanyiko wa uwajibikaji. Kadiri jukumu lina- vyokuwa la watu wengi bila kubainishwa nani anawajibika kwa nini, ndivyo kila mmoja ana- vyoweza kupunguza hisia ya wajibu binafsi.

Dhana nyingine ni social loafing, inayofa- fanua tabia ya baadhi ya watu kupunguza juhudi wanapofanya kazi katika kundi, hasa pale ambapo mchango wa kila mmoja hauwezi kutambuliwa au kupimwa kwa urahisi.

Pia, kiasili, binadamu wengi hupenda kuona

matokeo ya juhudi zao na kutambuliwa kwa mafanikio waliyoyapata. Mtu anapopewa jukumu maalumu na kulitekeleza vizuri, anapata hisia ya umiliki wa kazi, mafanikio na wajibu wa kuen- deleza kile alichokianzisha. Kwa baadhi ya watu, hali hiyo inaweza kupunguza ari ya kujituma kuliko pale ambapo wangekuwa na jukumu bin- afsi na uwajibikaji wa moja kwa moja.

Haimaanishi kamati hazina faida

Hii haimaanishi kwamba mfumo wa kamati hauna faida. Kinyume chake, ni mfumo mzuri wa kuleta ushirikishwaji, kukusanya mawazo mbalimbali, kujenga maamuzi ya pamoja na kuwapa wanachama nafasi katika uendesaji wa taasisi.

Hata hivyo, faida hizo hutegemea sana kiwango cha ushiriki na uwajibikaji wa wajumbe. Kamati yenye watu wenye ari, majukumu yaliyo wazi na utaratibu wa kufuatilia utekelezaji inaweza kufanya kazi vizuri. Lakini kamati inayotege- mea tu dhamira ya pamoja, bila uwajibikaji bin- afsi, inaweza kuwa mahali pa mikutano mingi na utekelezaji mdogo.

Utawala dhidi ya utendaji

Katika taaluma ya usimamizi wa taasisi, kuna tofauti kati ya utawala (governance) na utend- aji (management). Utawala unahusu kuweka sera, mwelekeo na kusimamia uwajibikaji, wakati utendaji unahusu kuhakikisha mipango inatekelezwa.

Kamati zinaweza kuwa na manufaa makubwa katika kujadili masuala, kutoa ushauri na kusi- mamia utekelezaji, lakini si lazima ziwe vyombo bora vya kuendesha shughuli za kila siku.

Hivyo basi, ni muhimu taasisi zitathmini mahi- taji yake kabla ya kuunda kamati. Si kila jambo muhimu linahitaji kamati ya kudumu. Tujiulize, je, tunahitaji kamati nyingi kama tulizonazo na je, kila kazi tunayozikabidhi kamati inafaa kutekelez- wa kwa mfumo wa kamati?

Chukulia kamati ya uchumi inayotarajiwa kubuni miradi na kutafuta mitaji, kusimamia uwekezaji na kuongeza mapato ya taasisi. Je, maju- kumu hayo yanaweza kutekelezwa kwa ufanisi kupitia mikutano ya mara chache ya wajumbe ambao hakuna anayewajibika moja kwa moja kwa matokeo?

Au kamati ya elimu inayotakiwa kuandaa mafunzo na kuboresha huduma za elimu. Je, majukumu hayo hayahitaji uratibu endelevu na mtu anayejulikana wazi kuwa ndiye mwenye dha- mana ya kuhakikisha kazi zinafanyika?

Hapa ndipo tunapopaswa kuutazama mfumo mwingine wa uendesaji wa taasisi: mfumo wa idara au kurugenzi (Departmental/Directorate- Based Structure).

Mfumo wa idara/ kurugenzi

Katika mfumo huu, taasisi inakuwa na vitengo maalumu, kwa mfano Kurugenzi ya Elimu, Kuru- genzi ya Uchumi, Kurugenzi ya Afya na Kurugenzi ya Mipango.

Kila kurugenzi ina kiongozi anayewajibika moja kwa moja kwa malengo, mipango na utekelez- aji wa shughuli zake. Mgawanyo huo unaweza kurahisisha uratibu, uwajibikaji na upimaji wa matokeo. Tofauti yake muhimu ni kwamba, bada- la ya jukumu kuwa la wajumbe wote kwa ujumla, kuna mtu anayejulikana kuwa ndiye mwenye dhamana ya kuhakikisha kazi inafanyika. Akifani- kiwa, mchango wake unatambulika; akishindwa, anawajibika kutoa maelezo.

Hata hivyo, mfumo huu nao si dawa ya kila tatizo. Unaweza kuongeza gharama na ikiwa hau- tasimamiwa vizuri, unaweza kupunguza ushiriki wa wanachama.

Aidha, kubadilisha jina la kamati na kuiita kuru- genzi hakutaleta mabadiliko ikiwa watu wale wale wataendelea kufanya kazi kwa utaratibu ule ule, bila malengo, mamlaka na uwajibikaji ulio wazi.

Mfumo chotara

Kutokana na changamoto za kila mfumo, kuna umuhimu wa kufikiria mfumo unaochanganya kamati na kurugenzi, kila moja ikiwa na maju- kumu maalumu.

Katika mfumo huo, viongozi wakuu wanawa- jibika kwa mwelekeo wa taasisi, sera na usimam- izi. Kamati zinatoa ushauri, zinachambua mipan- go na kuhakikisha sauti za wanachama zinasikika, huku idara au kurugenzi zikitekeleza shughuli.

Kwa taasisi zenye rasilimali chache, si lazima kila kurugenzi iwe na wafanyakazi wanaolipwa. Inawezekana kutumia wakurugenzi au waratibu wa kujitolea, mradi wawe na majukumu maalu- mu, mamlaka yanayoeleweka, mipango kazi na utaratibu wa kupima matokeo.

Katika taasisi zetu za kidini, tunasisitiza sana ikhlasi, kujitolea, amana na uwajibikaji. Hayo ni maadili muhimu ambayo hatupaswi kuyaacha. Lakini maadili hayo peke yake hayawezi kuchu- kua nafasi ya mfumo mzuri wa utendaji bila kuwe- ka mazingira yanayochochea uwajibikaji binafsi.

Nimalize kwa kusema, huenda tatizo letu si ukosefu wa watu wenye moyo wa kujitolea, bali ni kuendelea kutumia mifumo inayofifisha uwa- jibikaji binafsi na kupunguza ari ya kujituma. Ni wakati wa taasisi zetu kufanya tathmini ya kina kuhusu mifumo yao ya uongozi na utendaji. Si lazima kila taasisi iondoe kamati na kuanzisha kurugenzi, lakini ni lazima tujiulize kama mifu- mo tuliyonayo inatimiza mahitaji ya sasa.

Kama mwanao anapata matokeo dhaifu darasani, fanya haya...

KILA mzazi anatamani mtoto wake afanye vizuri shuleni, lakini matokeo yakiwa tofauti na matarajio, furaha hiyo inaweza kugeuka kuwa hasira, huzuni na kukata tamaa. Baadhi ya wazazi hukimbilia kumkaripia mtoto, kumwadhibu au kumlinganisha na wenzake. “Mbona mwenzako anafaulu na wewe unafeli?” “Husomi!” “Hivi akili zako ziko wapi?” Lakini je, tumewahi kujiuliza athari za maneno haya kwa mtoto anayejitahidi kadiri ya uwezo wake? Katika saikolojia ya elimu, kufanya vibaya darasani si lazima kuwe ishara ya uvivu au uwezo mdogo wa kufikiri. Mtoto anaweza kuwa na msingi dhaifu wa maarifa, changamoto ya ujifunzaji, mbinu zisizomfaa au matatizo ya kihisia yanayoathiri uwezo wake. Makala iliyochapishwa na Jarida la Absolutely Education la Uingereza inataja athari za kukatishwa tamaa ikiwemo mtoto kuamini kwamba hawezi kufanikiwa na kuanza kufikiria kuacha kusoma. Baadhi, huanza kujiiondoa katika shughuli za kujifunza. Wengine huonyesha hasira, hukaa kimya au kupoteza kabisa hamasa ya kushiriki darasani. Hivyo, mzazi anapogundua mtoto wake anafanya vibaya, anapaswa kuchukua hatua zifuatazo.

Mosi, tafuta chanzo cha tatizo badala ya kulaumu

Watoto hawashindwi kitaaluma kwa sababu zinazofanana. Mmoja anaweza kuwa na matatizo ya kusoma, mwingine kuelewa hesabu, huku mwingine akishindwa kuzingatia masomo kutokana na mazingira au changamoto za kihisia.

Wengine wanaweza kuwa na matatizo ya kuona, kusikia au changamoto maalumu za ujifunzaji kama dyslexia, inayohusishwa na ugumu wa kusoma.

Zungumza na mwalimu, chunguza kazi zake na msikilize mtoto mwenyewe. Ikibidi, tafuta ushauri wa kitaalamu.

Pili, usimlinganishe na watoto wengine

Mtoto anayesikia kila siku kwamba wenzake ni bora kuliko yeye anaweza kupoteza kujiamini na kuanza kuchukua shule.

Badala ya kumlinganisha na mwanafunzi anayepata alama 90, linganisha maendeleo yake mwenyewe. Ikiwa alikuwa anapata alama 20 na sasa anapata 35, huo ni mwanzo unaostahili kutambuliwa.

Mtoto anapaswa kuelewa kwamba kushindwa mtihani hakumaanishi hana uwezo wa kujifunza.

Tatu, rudi kwenye msingi wa maarifa

Mara nyingi mtoto hushindwa mada mpya kwa sababu hakuelewa vizuri mada za awali.

Kwa mfano, mtoto asiyejua kuzidisha anaweza kupata shida kugawanya namba. Anayeshindwa kutambua herufi na sauti zake anaweza kushindwa kusoma maneno.

Kwa kutambua hilo, wataalamu wanashauri ufundishaji wa hatua kwa hatua, kuanzia maarifa ya msingi na kuongeza ugumu kadiri mtoto anavyoelewa.

Nne, badilisha mbinu za kufundisha

Kusoma kitabu na kusikiliza maelezo pekee hakuwasaidii watoto wote kwa kiwango sawa.

Mtoto anaweza kuelewa hesabu kwa kutumia mawe, vijiti au matunda kuliko kwa kungalia namba ubaoni.

Tumia mifano ya maisha, picha, mazungumzo na shughuli za vitendo kulingana na somo na mahitaji yake. Lengo ni kumsaidia kuelewa, si kukariri majibu.

Tano, mpe muda maalumu wa kumsaidia

Wataalamu wa ujifunzaji wanashauri vipindi vifupi vinavyofanyika mara kwa mara, badala ya kumchosha mtoto kwa masaa mengi ya

masomo bila mapumziko.

Unaweza kuanza na dakika 15 hadi 20 kwa siku, ukizingatia umri na uwezo wake. mFundisha jambo moja, mpe nafasi ya kufanya mazoezi na rudia maarifa aliyojifunza.

Ikiwezekana, msaada wa mwalimu wa ziada unaweza kuwa na manufaa, hasa unapolenga udhaifu maalumu badala ya kuongeza tu kazi nyingi.

Sita, jenga kujiamini kwake

Mtoto anayeshindwa mara kwa mara anaweza kujenga imani kwamba hata akijitahidi hata-pata mafanikio.

Katika saikolojia, mtazamo unaoitwa growth mindset unasisitiza kwamba uwezo unaweza kukuzwa kupitia kujifunza, juhudi, mbinu zinazofaa na msaada.

Badala ya kumwambia, “Wewe huwezi hesabu,” mwambie, “Bado hujaelewa vizuri, lakini tutajifunza pamoja.”

Msifie kwa juhudi na maendeleo ya kweli, huku ukimwelekeza anapokosea.

Saba, tambua vipaji vyake vingine

Aghlab, watoto wengi wanaopata ugumu katika kuelewa masomo, wana vipaji vingine vikubwa sana ikiwemo katika kazi za vitendo, ubunifu, michezo, ufundi, uongozi, ushawishi na kadhalika. Tambua uwezo katika maeneo hayo. Mafanikio hayo yanaweza kumjengea kujiamini na kuona ana thamani ya kipekee, ingawa pia usiache kumsaidia katika masomo.

Nane, shirikiana na walimu

Mzazi na mwalimu hawapaswi kulaumiana. Wana jukumu la kushirikiana kutambua matatizo, kuweka malengo yanayotekelezeka na kufuatilia maendeleo.

Hatimaye, tukumbuke kwamba nafasi ya mtoto darasani ni kipimo cha matokeo ya masomo katika wakati fulani, si kipimo cha thamani yake au hatima ya maisha yake.

Mtoto aliye wa mwisho darasani hahitaji kukatishwa tamaa. Anahitaji kueleweka, kuaminiwa na kusaidiwa ili aweze kusonga mbele. Tusikazanie tu swali, “Kwa nini mtoto huyu anafeli?” Tujiulize pia, “Ni nini kinamzuia kujifunza, na tunaweza kumsaidiaje?”

Mwalimu, peleka watoto wakajifunze nje ya darasa

TUNAPOZUNGUMZIA elimu, wengi wetu tunafikiria darasa lenye madawati, ubao, vitabu na mwalimu anayefundisha huku wanafunzi wakisikiliza na kuandika. Kwa muda mrefu, mfumo huu umekuwa njia kuu ya kufundisha watoto katika shule zetu.

Hata hivyo, wataalamu wa elimu wanatukumbusha kwamba kujifunza hakupaswi kuishia ndani ya kuta nne za darasa. Mazingira yanayotuzunguka yanaweza kuwa darasa jingine lenye fursa nyingi za kuwajengea watoto maarifa, ujuzi na uwezo wa kutatua matatizo.

Mtazamo huu unajulikana kitaalamu kama Outdoor Education, yaani elimu inayotolewa kupitia shughuli za kujifunza nje ya darasa.

Mtaalamu wa elimu Phyllis Ford, katika andiko lake Outdoor Education: Definition and Philosophy, anaeleza elimu hii kuwa kujifunza katika mazingira ya nje, kujifunza kuhusu mazingira hayo na kujifunza namna ya kuyatunza na kuyatumia kwa uwajibikaji.

Hii ina maana kwamba elimu ya nje si lazima iwe safari ya mbali, kupanda milima au kwenda hifadhi za taifa. Inaweza kufanyika katika bustani ya shule, shamba, soko, ufukweni, kiwandani au mazingira mengine yanayomzunguka mtoto.

Kwa mfano, badala ya mwalimu kueleza

kwa maneno pekee namna mimea inavyoota, anaweza kuwapeleka wanafunzi bustanini kupanda mbegu, kuzimwagilia na kufuatilia ukuaji wake.

Hapo mtoto hajifunzi tu hatua za ukuaji wa mimea, bali pia anajenga tabia ya uwajibikaji, uvumilivu na utunzaji wa mazingira.

Si kwa sayansi pekee

Elimuyanjanaweza kutumika kufundishia masomo mengi, si sayansi pekee.

Kwa mfano, somo la hesabu linaweza kufundishwa kwa kutumia mawe, vijiti au vitu vingine vinavyopatikana katika mazingira. Katika lugha, wanafunzi wanaweza kutembelea sehemu fulani na baadaye kuandika insha kuhusu walichokiona.

Kwa upande wa jioografia, wanafunzi wanaweza kuchunguza miinuko, udongo, mito na matumizi ya ardhi badala ya kutegemea picha za vitabuni pekee.

Faida mojawapo ya mbinu hii ni kuwasaidia watoto kuunganisha nadharia wanazofundishwa na maisha halisi.

Mtoto anayesoma kuhusu mmomonyoko wa udongo anaweza kushindwa kuelewa vizuri kwa maelezo ya darasani. Lakini anapoonyeshwa eneo ambalo maji yamesomba udongo, dhana hiyo inaweza kuwa rahisi zaidi kuielewa.

Elimu ya nje pia inaweza kukuza ushirikiano na ujuzi wa kijamii.

Michael Becker, katika makala yake 5 Benefits of Outdoor Education iliyochapishwa na Edutopia mwaka 2016, anaeleza uzoefu wa programu ya wanafunzi wa darasa la sita nchini Marekani waliokuwa wakijifunza kupitia shughuli za nje.

Katika programu hiyo, wanafunzi walishiriki kupika, kusafisha mazingira, kuandaa chakula na kutekeleza majukumu mbalimbali kwa pamoja.

Shughuli hizo ziliwapa nafasi ya kujifunza kuwajibika, kushirikiana na kutatua matatizo bila kutegemea mwalimu kuwafanyia kila kitu.

Aidha, kujifunza nje kunaweza kuwasaidia watoto wanaopata ugumu wa kuzingatia masomo wanapokaa darasani kwa muda mrefu.

Baadhi ya tafiti zinahusisha muda unao-tumika katika mazingira ya asili na kupungua kwa msongo wa mawazo pamoja na kuboreka kwa umakini. Hata hivyo, manufaa hutegemea aina ya shughuli, mazingira na mahitaji ya mtoto.

Elimu hii pia inaweza kusaidia kutambua vipaji ambavyo havionekani kirahisi katika mitihani ya kawaida. Mtoto anayepata alama ndogo darasani anaweza kuonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza wenzake, kutengeneza vifaa, kutunza mimea au kutatua matatizo ya vitendo.

Kwa hiyo, shughuli za nje zinaweza kuwa fursa ya kukuza kujiamini na kutambua uwezo tofauti wa wanafunzi.

Hali ilivyo Tanzania

Kwa shule zetu nchini Tanzania, utekelezaji wa elimu ya nje hauhitaji kuanza kwa bajeti kubwa. Shule inaweza kutenga bustani ya mafunzo, kuandaa matembezi ya kielimu katika mazingira ya karibu au kuwapeleka wanafunzi kutembelea shughuli za uzalishaji na huduma katika jamii.

Kwa mfano, ziara sokoni inaweza kuwa-fundishawatoto hesabu, biashara, mawasiliano na matumizi ya fedha. Kutembelea shamba kunaweza kuwafundisha sayansi, kilimo na uhifadhi wa mazingira.

Hata hivyo, shughuli hizo zinapaswa kuwa na malengo ya kielimu, maandalizi ya kuto-sha, usimamizi wa walimu na tahadhari za usalama.

Si kila matembezi nje ya shule ni elimu. Kinachoyafanya kuwa shughuli ya kielimu ni kuwepo kwa malengo maalumu, ushiriki wa wanafunzi na tathmini ya kile walichoji-funza.

Vilevile, elimu ya nje haikusudiwi kuchukua nafasi ya darasa, vitabu au walimu. Lengo ni kuimarisha ujifunzaji kwa kuwapa watoto nafasi ya kuona, kufanya majaribio, kuuliza maswali na kujifunza kutokana na uzoefu.

Kwa muda mrefu, tumekuwa tukipima mafanikio ya elimu kwa kuangalia zaidi uwezo wa mwanafunzi kujibu maswali ya mtihani. Lakini elimu bora inapaswa pia kumwandaa mtoto kuelewa mazingira yake, kushirikiana na wengine, kufikiri kwa kujitegemea na kutumia maarifa katika maisha.

Ni wakati wa shule na wazazi kutambua kwamba elimu haipo vitabuni na mada-rasani pekee. Mazingira yanayotuzunguka nayo ni sehemu muhimu ya kujifunzia.

Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA

7

Kuzungumza na AI: Maelekezo mazuri ndiyo nusu ya kazi

Watu wawili wanaweza kutumia mfumo uleule wa akili bandia (AI), lakini wakapata majibu yenye tofauti kubwa. Mara nyingi sababu si uwezo wa mfumo, bali namna walivyouliza.

AI inahitaji maelekezo. Maelekezo hayo huitwa prompt. Kwa Kiswahili rahisi, ni kile unachoandika au kusema ili kuieleza AI unachotaka ikufanyie.

Ukiandika, “Nisaidie kuhusu habari hii,” umeacha mambo mengi wazi. AI haijui wewe ni nani, habari inamhusu nani, unataka msaada wa aina gani, hadhira yako ni ipi, wala mipaka gani inapaswa kuzingatia.

Kadiri maelekezo yanavyokuwa wazi, ndivyo uwezekano wa kupata msaada wenye maana unavyoongezeka.

Usiambie tu unachotaka, ipe mazingira

Tuseme mwandishi anaandaa habari kuhusu ukosefu wa ajira kwa vijana. Anaweza kuuliza: “Nipe maswali kuhusu ukosefu wa ajira.” Atapata majibu. Lakini yanaweza kuwa ya jumla mno.

Anaweza badala yake kusema: “Ninaandaa habari kwa wasomaji wa Tanzania kuhusu changamoto za vijana kupata ajira baada ya kuhitimu. Nisaidie kuandaa maeneo sita ya kuchunguza na maswali ya kuwauliza wahitimu, waajiri na wataalamu wa soko la ajira. Usinitungie takwimu wala madai.”

Hapo AI imepewa kazi, mazingira, hadhira na mipaka. Uwezekano wa kupata jibu linalofaa unaongezeka.



Eleza kazi unayotaka ifanye

AI inaweza kusaidia katika mambo mengi. Inaweza kupendekeza maswali, kupanga dondoo, kutafuta mapengo katika rasimu, kufupisha maandishi au kupendekeza miundo tofauti. Tatizo huanza mwandishi anapoiambia kufanya kila kitu kwa wakati mmoja.

Badala ya kusema, “Boresha habari hii,” ni bora kueleza unachotaka kuboreshwa. Je, unataka kupunguza marudio? Kurahisisha lugha? Kubaini sehemu ambazo hazina chanzo? Kupendekeza kichwa? Au kuangalia kama mtiririko unaeleweka?

Maelekezo mahsusi yanampa mwandishi uwezo mkubwa zaidi wa kudhibiti matokeo.

Iambie kile isichopaswa kufanya

Hili ni muhimu sana katika uandishi wa habari. Mwandishi anaweza kusema: “Usiongeze taarifa ambayo haipo katika maandishi haya.” Anaweza kuongeza: “Usibadilishe nukuu,” au “Usitengeneze majina, takwimu na vyanzo.”

Hii haimaanishi kwamba AI haitakosea. Lakini kuweka mipaka kunapunguza nafasi

ya mfumo kwenda mbali na kazi uliyoikusudia. Kwa hiyo, maelekezo mazuri hayataji tu unachotaka. Yanataja pia kile ambacho hutaki.

Usikubali jibu la kwanza kuwa la mwisho

Mazungumzo na AI hayapaswi kuishia kwenye swali moja na jibu moja.

Ukipata jibu pana sana, unaweza kusema: “Fupisha.” Ikiwa limekosa upande fulani, unaweza kuuliza: “Ni kundi gani muhimu hujalitaja?” Ikiwa mapendekezo yanafanana, unaweza kusema: “Nipe mitazamo tofauti zaidi.”

Hii ndiyo faida ya kuizungumza AI kama mchakato. Mwandishi anaweza kuanza na wazo, kuona majibu, kuyachunguza, kuyauliza maswali zaidi na hatimaye kuchukua yale yenye manufaa. Hata hivyo, kila hatua inahitaji uamuzi wake mwenyewe.

Maelekezo mazuri hayawezi kuifanya AI iwe chanzo cha ukweli

Hapa kuna mpaka muhimu. Unaweza kuandika maelekezo bora kabisa na bado AI ikakosea. Inaweza kutoa tarehe isiyo sahihi, jina lisilokuwepo au rejea ambayo inaonekana ya kuaminika lakini si halisi.

Kwa hiyo, uwezo wa kuandika maelekezo mazuri hauondoi wajibu wa kuhakiki. Maelekezo yanaweza kuboresha ubora wa msaada, lakini hayawezi kuhakikisha ukweli wa kila jibu.


Jifunze kuipa kazi ndogo ndogo

Njia nzuri ya kuitumia AI ni kugawa kazi. Badala ya kumpa habari nzima na kusema, “Fanya kila kitu,” mwandishi anaweza kwanza kuitumia kuangalia muundo. Baa-daye akaitumia kuonyesha marudio. Kisha akaiomba kupendekeza vichwa. Kila hatua inakuwa rahisi kuikagua.

Hii pia inamsaidia mwandishi kubaki kwenye usukani. Anajua AI imefanya nini na anaweza kuona kwa urahisi sehemu inayohitaji kurekebisha.

Kwa ufupi, hoja yangu muhimu leo ni kuwa Usiombie AI tu ikufanyie kitu. Ieleze kazi, mazingira, mipaka na aina ya jibu unalotaka.

Lakini hata maelekezo mazuri hayawezi kuondoa hatari kubwa zaidi ya AI: inaweza kutoa taarifa isiyo sahihi huku ikiieleza kwa kujiamini. Hilo ndilo tutakaloangalia katika makala inayofuata.



Jinsi ya kushinda uraibu na kurejesha maisha yako

URAIBU wa pombe, dawa za kulevya, kamari na tabia nyingine zinazojenga utegemezi unaweza kuharibu afya, mahusiano ya kifamilia, uchumi na maisha ya mtu kwa ujumla. Wengi wanaotumbukia katika hali hii hutamani kuacha, lakini hushindwa licha ya kufahamu madhara wanayopata.

Kwa baadhi ya watu, hali hiyo hutafsiriwa kuwa ukosefu wa nidhamu, udhaifu wa tabia au kutokuwa na nia ya kweli ya kubadilika. Hata hivyo, wataalamu wa afya ya akili wanaeleza kwamba uraibu ni tatizo tata linaloweza kuathiri mfumo wa ubongo unaohusika na kutafuta raha, kufanya maamuzi na kudhibiti misukumo.

Kwa mujibu wa Cleveland Clinic, kupona uraibu ni mchakato unaohitaji muda, msaada na mabadiliko ya kitabia. Si jambo linalomalizika kwa mtu kuamua tu kuacha kutumia kile alichokizoea.

Dkt. Jared Harp, mtaalamu wa magonjwa ya akili na uraibu katika Cleveland Clinic, anaeleza hatua tano zinazoweza kumsaidia mtu kuelewa safari ya kupona.

Hatua za tano hadi kuacha uraibu

Mosi, kutotambua kwamba una tatizo

Katika hatua hii, mtu anaweza kutumia pombe au dawa za kulevya kupita kiasi lakini akaamini kwamba hana tatizo.

Anaweza kusema, “Ninaweza kuacha wakati wowote,” au “Mimi situmii sana kama wengine.”

Hata anapoonyeshwa madhara ya tabia yake, anaweza kuyapuza au kutafuta sababu za kujitetea. Hivyo, hatua muhimu ni kumsaidia kutambua madhara bila kumdhaliisha.

Pili, kuanza kutafakari mabadiliko

Hapa mtu anaanza kujiuliza kama tabia yake inamletea manufaa au madhara.

Anaweza kutambua kwamba pombe inaharibu ndoa yake au kamari inamaliza kipato chake, lakini bado akaamini tabia hiyo inampunguzia msongo wa mawazo.

Hii ni hatua ya mvutano wa ndani, ambapo mtu anatamani kubadilika lakini bado anahofia kuacha.

Tatu, kujiandaa kubadilika

Mtu anapokubali kwamba madhara yamezidi manufaa anayoyatarajia, huanza kupanga hatua za kuchukua.

Anaweza kuzungumza na mtu anayemwamini, kutafuta kituo cha matibabu, kuwasiliana na mshauri au kuandaa mpango wa kuacha.

Hata hivyo, kwa mtu mwenye utegemezi wa pombe au baadhi ya dawa, kuacha ghafla kunaweza kubaabisha dalili hatari za kujiondoa. Ni muhimu kupata ushauri wa kitabibu kabla ya kufanya mabadiliko makubwa.

Nne, kuchukua hatua

Katika hatua hii, mtu anaanza kutekeleza mpango wake wa kupona.

Anaweza kuanza matibabu, kuhudhuria ushauri nasaha, kujiunga na kundi la watu wanaosaidiana kuacha uraibu au kubadilisha mazingira yanayomshawishi kurudia tabia hiyo.

Hatua hii inaweza kuwa ngumu kutokana na hamu kali ya kutumia kile alichokizoea. Ndiyo maana msada wa wataalamu, familia na marafiki ni muhimu.

Tano, kudumisha mabadiliko

Kuacha uraibu kwa siku chache au miezi kadhaa hakumaanishi kwamba hatari ya kurudia imeondoka kabisa.

Mtu anahitaji kuendelea kujenga tabia zinazomsaidia kudhibiti msongo wa mawazo na kuepuka mazingira yanayochochea uraibu.

Wataalamu wanasisitiza kwamba hatua hizi hazifuatani kwa mpangilio uleule kwa kila mtu. Mtu anaweza kusonga mbele, kurudi nyuma na kuanza tena.

Lakini pamoja na hatua hizo, kuna mazoea yanayoweza kusaidia kudumisha mafanikio.

Mbinu na mikakati mahsusi

Kwanza, epuka mazingira yanayokushawishi

Ikiwa ulikuwa unatumia dawa za kulevya ukiwa na marafiki fulani, punguza au acha kukutana nao katika mazingira hayo.

Vivyo hivyo, mtu anayepambana na uraibu wa kamari anaweza kuhitaji kuondoa programu za kubashiri na kujiepusha na matangazo yanayomshawishi kucheza.

Pili, jenga tabia mpya zenye manufaa

Kwa mujibu wa Alvarado Parkway Institute, mazoezi yamwili, lishe bora, kupumzika na kushiriki shughuli zinazopendwa vinaweza kusaidia safari ya kupona.

Badala ya kutumia pombe unapokasirika, unaweza kutembea, kufanya mazoezi au kuzungumza na mtu unayemwamini.

Lengo ni kujifunza njia salama za kukabiliana na hisia ambazo hapo awali zilikuwa zinakusukuma kwenye uraibu.

Tatu, shirikisha watu wanaokujali

Familia na marafiki wanaweza kutoa faraja, kukutia moyo na kumsaidia kufuatilia maendeleo.

Hata hivyo, msaada haupaswi kumaanisha kufumbia macho tabia zinazodhuru. Wanaokusaidia wanapaswa kuweka mipaka yenye afya huku wakikuunga mkono katika matibabu.

Namna ya kukabiliana na huzuni na msongo wa mawazo

HUZUNI na msongo wa mawazo ni sehemu ya maisha ambayo karibu kila binadamu hupitia. Kufiwa na mpendwa, kupoteza kazi, matatizo ya ndoa, madeni, maradhi au kushindwa kutimiza matarajio kunaweza kumfanya mtu akose furaha, matumaini na hata usingizi. Hata hivyo, wataalamu wa saikolojia na mafundisho ya Kiislamu wanakubaliana kwamba mwanadamu anaweza kuchukua hatua za kukabiliana na hali hizo.

Kwa mujibu wa Shirika la Huduma za Afya la Uingereza (NHS), huzuni inaweza kusababisha uchovu, wasiwasi, hasira na kupungua kwa kujiamini. Hata hivyo, huzuni ya kawaida hutofautiana na mfadhaiko wa akili (depression), ambao unaweza kuhitaji matibabu.

Katika Uislamu, kuhuzunika si dhambi wala ishara ya udhaifu wa imani. Qur'an inasimulia jinsi Nabii Yaqub (amani ya Allah iwe juu yake) alivyohuzunika kutokana na kumpoteza mwanawe Yusuf, akisema: "Hakika mimi namshitakia Mwenyezi Mungu huzuni yangu na masikitiko yangu." [Qur'an, 12:86].

Hivyo, huzuni ni hisia ya kibinadamu inayohitaji kueleweka na kushughulikiwa kwa njia zinazofaa. Zifuatazo ni hatua zinazoweza kusaidia.

Mosi, kubali hisia zako badala ya kuzificha

Watu wengine hujilazimisha kuonekana wenye furaha hata wanapoumia ndani. Wataalamu wanaeleza kwamba kukubali huzuni na kuitambua sababu yake ni hatua muhimu ya kukabiliana nayo.

Usione aibu kulia au kueleza maumivu yako. Hata Mtume Muhammad (Allah

amshushie rehema na amani) alilia alipofiwa na mwanawe Ibrahim, akionyesha kwamba machozi na huzuni havipingani na subira.

Pili, zungumza na mtu unayemwami-ni

Kuweka matatizo moyoni kunaweza kuongeza hisia za upweke. Kuzungumza na rafiki, ndugu, mwenzi au mshauri kunaweza kupunguza mzigo wa kihisia.

Uislamu unahimiza kusaidiana katika mambo mema. Kwa hiyo, kumfariji mwenye huzuni na kumsikiliza kwa huruma ni sehemu ya mshikamano wa kijamii.

Si lazima anayekusikiliza awe na majibu yote. Wakati mwingine mtu huhitaji kusikilizwa tu.

Tatu, pata utulivu kupitia ibada na kutafakari

Wataalamu wa afya ya akili wanapendekeza mbinu za kutuliza mawazo na kuelekeza fikra katika wakati uliopo.

Kwa Muislamu, swala, dua, dhikri na kusoma Qur'an vinaweza kuwa njia za kupata faraja ya kiroho. Qur'an inasema: "Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutua." [Qur'an, 13:28].

Hata hivyo, ibada haipaswi kuchukuliwa kuwa mbadala wa matibabu kwa mtu mwenye ugonjwa wa akili unaohitaji msaada wa kitaalamu.

Nne, tunza afya yako ya mwili

Wataalamu wanashauri kufanya mazoezi, kula chakula bora na kupata usingizi wa kutosha ili kusaidia kuboresha hali ya kihisia.

Kutembea, kufanya kazi za nyumbani au kutumia muda katika mazingira ya asili kunaweza kupunguza msongo wa mawazo.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alifundisha umuhimu wa kuupa mwili haki yake, akisisitiza uwiano kati ya ibada, mapumziko na majukumu mengine.

Tano, andika mawazo yako na hesabu

neema ulizonazo

Kwa mujibu wa wataalamu kuandika hisia kunaweza kusaidia kutambua kinachosababisha huzuni. Unaweza kuandika matatizo yanayokusumbua pamoja na mambo mazuri katika maisha yako.

Katika Uislamu, kushukuru ni jambo muhimu. Hata unapopitia matatizo, kutambua neema zilizopo kunaweza kusaidia kujenga matumaini bila kupuuza maumivu yako.

Sita, chukua hatua ndogo na uwe na subira

Usijilazimishe kutatua matatizo yote kwa siku moja. Anza na mambo yaliyo ndani ya uwezo wako.

Qur'an inatukumbusha: "Hakika pamoja na uzito upo wepesi." [Qur'an, 94:5-6]. Subira haimaanishi kukaa bila kuchukua hatua. Inapaswa kuambatana na juhudi, kupanga upya maisha na kutafuta ufumbuzi.

Saba, epuka njia zinazoongeza matatizo

Baadhi ya watu hukimbilia pombe, dawa za kulevya, kamari au matumizi yasiyo ya lazima ili kusahau huzuni. Njia hizo zinaweza kutoa nafuu ya muda mfupi lakini kuongeza matatizo ya kiafya, kifedha na kijamii.

Badala yake, tafuta shughuli zenye manufaa, dumisha mahusiano na epuka kujitenga kupita kiasi.

Nane, tafuta msaada wa kitaalamu inapohitajika

Ikiwa huzuni inaendelea kwa wiki mbiili au zaidi, inapunguza uwezo wa kufanya shughuli za kawaida au inaambatana na kukata tamaa, ni muhimu kumuona mtaalamu wa afya.

Mtu mwenye mawazo ya kujidhuru anahitaji msaada wa haraka.

Kutafuta matibabu hakupingani na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Kama tunavyotibu maradhi ya mwili, tunapaswa pia kushughulikia matatizo ya afya ya akili.